VIONGOZI WA WIZARA

Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb.)
WAZIRI

Mhe. Juliana D. Shonza (Mb.)
NAIBU WAZIRI

Susan P. Mlawi
KATIBU MKUU

Nicholas B. William
NAIBU KATIBU MKUU

YALIYOMO

ORODHA YA VIFUPISHO iv

1.0 UTANGULIZI 1

2.0 DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA 5

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2018/19 7

3.1 MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA 7

3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2018/19 11

3.2.1 SEKTA YA HABARI 11

3.2.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI 24

3.2.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA 33

3.2.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO 50

3.2.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA 61

4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA 62

5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 64

5.1 SEKTA YA HABARI 64

5.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI 66

5.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA 68

5.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO 72

5.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA 75

6.0 MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 76

6.1 Mapato 76

6.2 Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo 76

7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2019/20 77

8.0 SHUKRANI 78

VIAMBATISHO 80

ORODHA YA VIFUPISHO

AFCON	African Cup of Nations
BASATA	Baraza la Sanaa la Taifa
BAKITA	Baraza la Kiswahili la Taifa
BBC	British Broadcasting Corporation
BMT	Baraza la Michezo la Taifa
CECAFA	Confederation of East and Central Africa Football Associations
CHABATA	Chama cha Baiskeli Tanzania
CHAKUTA	Chama cha Kuogelea Tanzania
DTH	Direct to Home
DTT	Digital Terrestrial Television
DVBS	Digital Video Broadcasting System
DVD	Digital Video Disc
EACG	East African Community Games
IPSAS	International Public Sector Accounting Standards
ITV	Independent Television
JAMAFEST	Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni Festival
JICA	Japan International Cooperation Agency
NACTE	National Council for Technical Education
NBAA	National Board of Accountants and Auditors
NBC	National Bank of Commerce
NCAA	Ngorongoro Conservation Area Authority
OBFT	Open Boxing Federation of Tanzania
OPRAS	Open Performance Review and Appraisal System

SBL	Serengeti Breweries Limited
SHIMMUTA	Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma na Makampuni Binafsi Tanzania
TABSA	Tanzania Baseball and Softball Association
TADA	Tanzania Darts Association
TANAPA	Tanzania National Parks
TaSUBa	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo
TAWA	Tanzania Wildlife Authority
TBC	Tanzania Broadcasting Corporation
TCDC	Training Center for Development Cooperation
TCRA	Tanzania Communication Regulatory Authority
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TFB	Tanzania Film Board
TGU	Tanzania Golf Union
TSN	Tanzania Standard Newspapers
UCSAF	Universal Communication Services Access Fund
UKIMWI	Ukosefu wa Kinga Mwilini
UNESCO	United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
VVIP	Very Very Important Person
VVU	Virusi vya Ukimwi

HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/20

1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja ya kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena kwenye Bunge lako Tukufu tukiwa wenye afya na uzima. Nashukuru pia kwa kuijalia nchi yetu kubaki katika hali ya amani na utulivu. Aidha, sina budi kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri mnaonipa unaoniwezesha kutekeleza kikamilifu majukumu niliyokabidhiwa.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii pia kumshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniamini nisimamie Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kufuatilia kwa karibu maendeleo yake.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano ambao imeendelea kutoa kwa Wizara yangu chini ya uongozi wa Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, na makamu wake Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Chemba. Kamati hii ilijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2019/20 tarehe 29 Machi, 2019 na kuyapitisha kwa kauli moja. Wizara yangu itazingatia ushauri uliotolewa na Kamati katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya mwaka 2019/20.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** niwapongeze pia Wabunge waliojiunga na Bunge lako Tukufu au kurejea Bungeni, wengi wakiwa katika sura tofauti kichama. Wabunge hao ni Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chizza (Buyungu), Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava (Korogwe Vijijini), Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara (Ukonga), Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer (Monduli), na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka (Liwale). Wengine ni Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi (Ukerewe), Mheshimiwa

Pauline Philipo Gekul (Babati Mjini), Mheshimiwa Ryoba Chacha Marwa (Serengeti) na Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea (Temeke).

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie pia fursa hii kuvishukuru na kuvipongeza Vyombo vya Habari vya redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii kwa kuendelea kuhabarisha na kuelimisha umma, hususan kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano za kuwaletea wananchi maendeleo. Aidha, nivipongeze Vyama vya Wasanii, Vilabu na Mashirikisho ya Michezo, Msanii mmoja mmoja, Wanahabari na Wachezaji kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Wizara yangu ambao umewezesha mafanikio makubwa kufikiwa katika mwaka 2018/19. Niwaeleze kuwa Wizara na Taasisi zake zipo kwa ajili ya kuwahudumia na kukidhi matarajio yao na vilevile kuhakikisha mafanikio stahiki yanapatikana katika kazi wanazozifanya.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2018/19 Bunge lako Tukufu lilimpoteza mmoja wa Wabunge, Mheshimiwa Steven Hillary Ngonyani, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini. Nitumie fursa hii kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu, jamaa na wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini kwa kumpoteza mwakilishi wao. Aidha, nitumie fursa hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa Wasanii, Wanamichezo na

Wanahabari waliopoteza maisha katika kipindi hiki. Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. AMINA

8. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kyela kwa imani, upendo, uelewa na ushirikiano mkubwa wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu ki-Jimbo na ki-Taifa kwa mafanikio makubwa. Kupitia Bunge lako Tukufu naomba niwahakikishie Wana-Kyela kuwa tutaendelea kushirikiana ili kuhakikisha Jimbo linaendelea kupiga hatua za uhakika za maendeleo na kutatua changamoto zinazoibuka. Aidha, naishukuru familia yangu kwa upendo na ushirikiano inayonipa ambao umeniwezesha nyakati zote kutekeleza majukumu yangu kwa ari, weledi na ufanisi.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** sina budi kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Mhe. Juliana Daniel Shonza (Mb.), Naibu Waziri, Bibi Susan Paul Mlawi, Katibu Mkuu na Bw. Nicholas Benjamin William, Naibu Katibu Mkuu. Niwashukuru pia Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma, tija na ufanisi.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2018/19 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2019/20.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba yangu imegawanyika katika Sehemu nane (8). Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara; Sehemu ya Tatu inaelezea Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2018/19 na Sehemu ya Nne inaeleza changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya Tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2019/20; Sehemu ya Sita ni Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2019/20; Sehemu ya Saba ni Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka 2019/20 na Sehemu ya Nane ni Shukrani kwa Wadau mbalimbali wa Wizara.

2.0 DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA

12. ***Mheshimiwa Spika,*** Dira ya Wizara ni *kuwa na Taifa linalohabarishwa vizuri, lililoshamirika kiutamaduni, lenye kazi bora za Sanaa na lenye umahiri mkubwa katika michezo ifikapo Mwaka 2025.*

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Dhima ya Wizara ni *kuendeleza utambulisho wa Taifa kwa kuwezesha upatikanaji stahiki wa Habari, kukuza Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa lengo la kuleta maendeleo ya jamii kiuchumi.*

Majukumu ya Wizara

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mipango mbalimbali ya Serikali katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, Wizara inasimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi mbalimbali zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (TFB), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Aidha, Wizara inasimamia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kinachotoa mafunzo ya michezo na pia Kamati ya Maudhui ambayo Kimuundo ipo chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Vilevile, Wizara ina jukumu la kuimarisha rasilimaliwatu ili kuwezesha majukumu na malengo ya Wizara kufikiwa kwa ufanisi na tija.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2018/19

3.1 MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

3.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

15. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2018/19, Wizara ilikadiria kukusanya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Sabini na Saba, Mia Nane na Nne Elfu (Sh.1,077,804,000) kutokana na vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo, Shilingi Milioni Mia Sita Hamsini na elfu mbili (Sh.650,002,000) zilipangwa kukusanywa kutokana na viingilio katika Viwanja vya Taifa na Uhuru ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Shilingi Milioni Mia Tatu Tisini na Mbili, Mia Saba Ishirini na Sita Elfu, na Hamsini na Nane (Sh.392,726,058) sawa na asilimia 60 zilikusanywa. Aidha, Shilingi Milioni Mia Tatu Sitini na Tisa, na Elfu Mbili (Sh.369,002,000) zilipangwa kukusanywa kutokana na malipo ya usajili wa magazeti na majarida, ukodishaji wa ukumbi wa Mikutano katika Idara ya Habari-MAELEZO pamoja na mauzo ya vitambulisho vya waandishi wa habari na picha mbalimbali za Viongozi wa kitaifa ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Shilingi Milioni Mia Moja Ishirini na Saba, Mia Tatu Arobaini na Saba Elfu, Mia Tisa Ishirini na Tisa (Sh.127,347,929) sawa na asilimia 35 ya lengo zilikusanywa.

Kwa upande wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Chuo hicho kilipanga kukusanya Shilingi Milioni Hamsini na Nane, Mia Nane Elfu (Sh.58,800,000) ikiwa ni maduhuli yatokanayo na ada za wanafunzi. Hadi Machi, 2019 Chuo kilikusanya Shilingi Milioni Mia Mbili Arobaini na Tisa, Mia Saba Thelathini na Moja Elfu, Mia Moja na Kumi (Sh.249,731,110) sawa na asilimia 425 ya lengo. Kuonyeshwa mubashara kwa mechi za mpira wa miguu kupitia televisheni na *apps* za simu za mkononi ni sehemu ya sababu za kutofikiwa ipasavyo kwa malengo ya makusanyo ya maduhuli yatokanayo na shughuli za michezo.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Taasisi saba (7) zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni jumla ya Shilingi Bilioni Thelathini na Mbili, Milioni Mia Saba Sitini na Moja, Mia Sita Ishirini Elfu (Sh. 32,761,620,000) ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Tatu Sabini na Sita, Mia Nane na Tatu Elfu, Mia Nne Hamsini na Nne (Sh.14,376,803,454) zilikusanywa sawa na asilimia 44 ya lengo la mwaka. Kuongezeka kwa ushindani katika biashara za huduma za utangazaji *(electronic media)* ikiwemo magazeti (*print media*) kutokana na kasi ya ukuaji wa teknolojia katika Sekta ya habari hususan matumizi ya mitandao ya kijamii katika utoaji

wa matangazo, na baadhi ya wadau wa sanaa, filamu na michezo kutojitokeza ipasavyo kujisajili na kutambulika kisheria ni baadhi ya sababu zilizoathiri ukusanyaji wa mapato. Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutoa elimu kuhusu manufaa ya kujisajili.

3.1.2 Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2018/19, Wizara iliidhinishiwa Shilingi Bilioni Thelathini na Tatu, Milioni Mia Tatu Arobaini na Tisa, Mia Sita Sabini na Tano Elfu (Sh.33,349,675,000) ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Ishirini na Nne, Milioni Mia Sita Arobaini na Tisa, Mia Sita Sabini na Tano Elfu (Sh.24,649,675,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, zikijumuisha Mishahara Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Mbili Hamsini na Tatu, Mia Mbili Sitini na Tano Elfu (Sh.15,253,265,000) na Matumizi Mengineyo Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Tatu Tisini na Sita, Mia Nne na Kumi Elfu (Sh.9,396,410,000). Miradi ya Maendeleo iliidhinishiwa Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Saba (Sh.8,700,000,000).

18. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Machi, 2019 Wizara ilipokea Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tatu Thelathini na Tatu, Mia Sita Tisini Elfu, Mia Nne Sabini na Nane (Sh.20,333,690,478)

ambayo ni sawa na asilimia 61 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Moja Hamsini na Tisa, Mia Saba Themanini na Nne Elfu, Mia Nne Sabini na Nane (Sh.15,159,784,478) ni Matumizi ya Kawaida ambayo ni sawa na asilimia 62, ambapo Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Tisini na Mbili, Mia Moja Ishirini na Tatu Elfu, Mia Tatu Sabini na Nane (Sh.10,092,123,378) ni mishahara sawa na asilimia 66 na Shilingi Bilioni Tano, Milioni Sitini na Saba, Mia Sita Sitini na Moja Elfu, Mia Moja (Sh.5,067,661,100) ni Matumizi Mengineyo sawa na asilimia 54. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo kiasi kilichopokelewa ni Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Moja Sabini na Tatu, Mia Tisa na Sita Elfu (Sh.5,173,906,000) sawa na asilimia 59 kwa miradi ifuatayo:-

a) Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika iliyotengewa Shilingi Bilioni Moja (Sh.1,000,000,000), imepokea Shilingi Milioni Mia Tano (Sh.500,000,000) sawa na asilimia 50;

b) Mradi wa Eneo Changamani la Michezo uliotengewa Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano (Sh.1,500,000,000), umepokea Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Hamsini na Tatu, Mia Tisa na Sita Elfu (Sh.1,353,906,000) sawa na asilimia 90;

c) Mradi wa Upanuzi wa Usikivu-TBC uliotengewa Shilingi Bilioni Tano (Sh.5,000,000,000) umepokea Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tano (Sh.2,500,000,000) sawa na asilimia 50;

d) Mradi wa Habari kwa Umma uliotengewa Shilingi Bilioni Moja, na Milioni Hamsini (Sh.1,050,000,000), umepokea Shilingi Milioni Mia Sita Sabini (Sh.670,000,000) sawa asilimia 64; na

e) Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya uliotengewa Shilingi Milioni Mia Moja Hamsini (Sh.150,000,000) umepokea fedha zote sawa na asilimia 100.

3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2018/19

3.2.1 SEKTA YA HABARI

19. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Sekta ya habari ni pamoja na kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003; Sheria ya Huduma za Habari Na.12 ya mwaka 2016 na kuisemea Serikali, kwa kutumia njia anuai, kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati na shughuli mbalimbali za kuwaletea wananchi maendeleo.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu la kuisemea Serikali, jumla ya mikutano saba (7) na wanahabari kwa ajili ya kuwajulisha wananchi kuhusu utekelezaji au ufafanuzi wa shughuli za Serikali ilifanyika. Aidha, Msemaji Mkuu wa Serikali, licha ya mahojiano mbalimbali katika televisheni na redio za ndani ya nchi, alifanya ziara maalum ya kutembelea na kufanya mahojiano mubashara na wananchi kupitia redio 26 za kijamii katika Mikoa 13 ili kuhabarisha wananchi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali na kuwapa fursa ya kutoa mrejesho na kutoa kero zao lakini pia kubaini changamoto katika redio hizo. Mikoa iliyofikiwa ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Singida, na Tabora. Ziara hizi zitaendelea katika Mikoa mingine.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** vipindi vya "TUNATEKELEZA" vinavyoratibiwa na Idara ya Habari-MAELEZO na TBC ili kuwezesha Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Watendaji Wakuu wa Wizara/Taasisi kuelezea umma kuhusu utekelezaji wa Sera na Mikakati ya Serikali katika maeneo yao pamoja na fursa zilizopo viliendelea kuratibiwa. Jumla ya vipindi 17 vilivyohusisha viongozi hao viliratibiwa na kurushwa hewani kupitia TBC_1.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wananchi wanapata haki yao ya kupata habari kwa haraka na usahihi, kwa kushirikiana na Chama cha Maafisa Habari na Mawasiliano Serikalini (TAGCO), iliandaa Kikao Kazi kilichohusisha Maafisa Habari na Mawasiliano Serikalini 350. Kikao hicho kilichofanyika mwezi Machi, 2019 Jijini Mwanza na kufunguliwa na Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kililenga kuwanoa na kuwakumbusha wajibu wao wa kuhabarisha umma. Aidha, Mhe. Waziri Mkuu alisisitiza umuhimu wa waajiri kuwapatia vifaa na kuwashirikisha ipasavyo maafisa hao ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016 ambayo pamoja na mambo mengine inaelekeza kuanzishwa kwa vyombo mbalimbali ili kuwezesha utekelezaji wake ikiwemo kuundwa kwa Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Mafunzo ya Wanahabari. Mapendekezo ya wajumbe wa kuteuliwa kwenye Bodi yamekamilika kwa hatua za uteuzi kwa mujibu wa Sheria na taratibu. Kwa kuwa Baraza Huru la Habari linategemea kupata wanachama kutoka Bodi ya Ithibati, Baraza hilo litaundwa mara baada ya Bodi ya Ithibati kuteuliwa na kuanza kazi.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa utoaji wa leseni za machapisho, hadi kufikia Machi, 2019 jumla ya magazeti mapya saba (7) yalipewa leseni na leseni kwa magazeti 59 zilihuishwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya mwaka 2016. Hadi mwezi Machi, 2019, magazeti yaliyopewa leseni kwa ujumla tangu Sheria mpya ilipoanza kutekelezwa Mwaka 2017 ni 216 ambapo 42 ni ya taasisi mbalimbali za umma na 184 ya Sekta Binafsi.

Aidha, magazeti manane (8): *Tanzania Daima*, *Mwananchi, Nyakati, Sani, Kiu, Tanzanite, Jamvi la Habari* na *Kisiwa* yalipewa onyo kwa mdomo na/au kwa maandishi, na gazeti moja kuchukuliwa hatua kali zaidi za kufutwa kabisa (gazeti la TUNATEKELEZA) ambapo gazeti la *The Citizen* lilipewa adhabu ya kutochapishwa kwa siku saba (7) kwa kukiuka weledi na maadili ya uandishi wa habari na sheria za nchi licha ya kuonywa mara kwa mara.

Kielelezo Na. 1: Magazeti na Majarida Yaliyosajiliwa Hadi Machi, 2019



3.2.1.1 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) lilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 186 la Mwaka 2007 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992. Majukumu ya TBC ni kutoa huduma ya utangazaji kwa kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha. Shirika linamiliki vituo vitatu vya televisheni vya TBC_1, TBC_2 na TBC_3 *(Tanzania Safari Channel)* na kwa upande wa redio linamiliki idhaa tatu za TBC_{Taifa}, TBC_{FM}, na $TBC_{International}$. Aidha, TBC inamiliki studio za redio za Kanda zilizopo Arusha, Dodoma, Kigoma, Lindi na Songea. Vilevile,

ili kuendana na kasi ya ukuaji wa teknolojia ya Habari, Shirika lina mifumo ya utangazaji ya kielektroniki kama vile tovuti na programu tumizi (protu au *App)* ambapo redio zote na televisheni za TBC zinapatikana. Kupitia njia hii ya mawasiliano TBC inaonekana na kusikika Dunia nzima.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maagizo ya Serikali ya kuhamia Dodoma, TBC imeanza maandalizi ya ujenzi wa Makao Makuu yake na michoro imekamilika. Aidha, mkataba wa ukarabati wa Studio za redio na televisheni Jijini Dodoma ili kuhakikisha studio hizo zinaimarishwa na kuendana na mahitaji ya sasa ulisainiwa tarehe 4 Machi, 2019. Vilevile, TBC imeingia makubaliano na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa gharama ya Shilingi Bilioni 1.014 kwa ajili ya ujenzi wa Studio za redio Jijini Dodoma. Mkataba wa Makubaliano ulisainiwa tarehe 27 Oktoba, 2018.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini, TBC kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro (NCAA), Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Bodi ya Filamu Tanzania (TFB), na wadau wengine imeanzisha Chaneli ya Utalii *(Tanzania Safari Channel).* Chaneli

hiyo ilizinduliwa na Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 15 Desemba, 2018. Aidha, nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri Mkuu pamoja na taasisi wadau kwa mchango wao katika uanzishwaji na uendeshaji wa Chaneli hii.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na watanzania kuitazama Chaneli hiyo inayoonekana bure kupitia visimbuzi mbalimbali ili kujionea vivutio vyetu vya utalii vikiwemo utalii wa kitamaduni na kiasili. Mkakati uliopo ni kuhakikisha inapatikana kwenye visimbuzi vyote pamoja na mifumo ya mitandao ya kijamii. Natoa rai pia kwa wananchi kuvitembelea vivutio mbalimbali vya utalii.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanyika kupitia bajeti ya maendeleo, TBC imeendelea kupanua usikivu wa redio mwaka hadi mwaka. Usikivu umeongezeka kutoka Wilaya 87 mwaka 2017 (asilimia 54) hadi Wilaya 95 mwaka 2018 (asilimia 59) ya Wilaya zote 161. Kufikia Machi, 2019 Wilaya 102 (asilimia 63) zimefikiwa na matangazo ya redio na Mpango wa TBC ni kuhakikisha usikivu wa redio unafikia Wilaya 117 (asilimia 73) katika mwaka ujao wa fedha.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** TBC imekamilisha ukarabati wa studio za kuhifadhi kumbukumbu za waasisi wa harakati za ukombozi Kusini

mwa Bara la Afrika. Studio hizi zimekarabatiwa na kufungwa vifaa na mitambo itakayotumika katika kubadilisha na kuhifadhi taarifa zote zilizoko katika maktaba ya redio katika mfumo wa kidijiti *(digital archiving).* Mradi huu ambao ulikabidhiwa kwa TBC tarehe 27 Julai, 2018 umetekelezwa kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) pamoja na Umoja wa Ulaya (EU).

31. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuenzi utamaduni wetu na kudumisha uzalendo na historia ya Taifa letu, TBC imerejesha hewani baadhi ya maudhui ya vipindi vya iliyokuwa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD). Vipindi hivyo ni pamoja na **Ndivyo Ilivyokuwa, Mawazo ya Kizalendo, Wosia wa Baba na Michezo ya Redio ya waigizaji nguli wakiwemo Mzee Jongo, Kipara, Jangala, Mama Haambiliki na Mzee Hamisi Tajiri** ambavyo vimekuwa vikirushwa kupitia Idhaa ya TBC_{Taifa} na TBC_1 kwa upande wa televisheni kupitia kipindi cha **Kutoka Maktaba.**

3.2.1.2 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kupitia Kamati ya Maudhui ina jukumu la kusimamia na kufuatilia maudhui yanayorushwa na Vituo vya Utangazaji ikiwa ni pamoja na yale ya Kielektroniki (Maudhui Mitandaoni).

33. ***Mheshimiwa Spika,*** TCRA kwa kushirikiana na Kamati ya Maudhui iliendelea kuhamasisha utengenezaji na uzalishaji wa maudhui ya ndani yanayozingatia maadili, mila na desturi za Mtanzania. TCRA iliendesha semina mbalimbali kwa wadau wa utangazaji, Wahariri na Watayarishaji (Wasimamizi) wa vipindi vya redio na televisheni katika Mikoa ya Dar es Salaam, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Mara, Mbeya, Mwanza, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Songwe na Tanga. Jumla ya wadau 184 kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na 91 kutoka Kanda ya Ziwa walishiriki. Kamati ya Maudhui pia ilivitembelea vituo vya utangazaji kwenye Mikoa husika.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** elimu juu ya Kanuni za Maudhui mitandaoni, redioni na kwenye televisheni iliendelea kutolewa, ambapo mafunzo kwa wasanii na waandaaji wa maudhui ya filamu na muziki juu ya matumizi ya Kanuni hizo yalitolewa. Mafunzo hayo ambayo yalihusisha washiriki 100 yalifanyika tarehe 15 na 16 Agosti, 2018 na yalilenga kuwapa uelewa wa namna ya kuzingatia Kanuni hizo.

Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilikutana na viongozi wa Jiji la Dodoma kwa ajili ya kuhamasisha uanzishaji wa Redio za Kijamii. Mkutano huo ulifanyika tarehe 15-18 Januari, 2019.

Vilevile, semina kuhusu Kanuni hizi ilitolewa kwa Vituo vya Utangazaji vya redio na

televisheni katika Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Singida na Tabora tarehe 15 Januari, 2019 ambapo Waandishi wa Habari, Watangazaji, Wasimamizi wa vipindi na Waandaaji wa vipindi 27 walishiriki.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Vituo sita (6) vya televisheni, 15 vya redio na vituo 72 vinavyotoa huduma za maudhui mtandaoni vilipewa leseni. Aidha, hadi Machi, 2019 kulikuwa na vituo 163 vya redio, 36 vya televisheni na idadi ya waliojisajili kutoa huduma za maudhui mtandaoni ilikuwa ni 274. Kiambatisho Na. I kinabainisha vyombo vya habari vilivyosajiliwa mwaka 2010-2018. Vielelezo Na. 2 na Na. 3 hapa chini vinabainisha idadi ya vituo vya televisheni na redio vinavyomilikiwa na Serikali na Sekta Binafsi.

Kielelezo Na. 2: Vituo vya Televisheni Vilivyosajiliwa Hadi Machi, 2019



Kielelezo Na. 3: Vituo vya Redio Vilivyosajiliwa Hadi Machi, 2019



36. ***Mheshimiwa Spika,*** vikao vya kujadili uanzishaji wa mfumo wa utangazaji wa redio za kidijiti kati ya TCRA na wadau wa utangazaji vilifanyika. Vikao hivyo vilihusisha Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati. Lengo ni kupata mfumo sahihi utakaotumika kutoa huduma za utangazaji kwa njia ya kidijiti.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Maudhui ya TCRA ilifanya ziara kwenye vituo vya utangazaji katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na Kanda ya Ziwa iliyolenga kubaini changamoto zinazowakabili wafanyakazi, kukutana na Wamiliki na kushauri kuhusu maslahi bora na mikataba yenye tija kwa wafanyakazi. Ziara hizi ambazo zilifanyika tarehe 27 Agosti hadi 10

Septemba, 2018 katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na tarehe 24 Februari hadi 09 Machi, 2019 katika Kanda ya Ziwa zililenga pia kuwakumbusha wamiliki wa vyombo vya utangazaji kuhakikisha wafanyakazi wote wanaohusika katika kuandaa na kutangaza wana sifa za kitaaluma kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari Na.12 ya Mwaka, 2016.

3.2.1.3 Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)

38. ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu kubwa la Kampuni hii ni kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha wananchi kwa njia ya magazeti. Magazeti yanayochapishwa na Kampuni hii ni Daily News, Sunday News, HabariLeo na SpotiLeo. Kampuni hutumia pia tovuti, mitandao ya kijamii kama vile *Twitter, Facebook,* na *Youtube* kuhabarisha umma.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni imeendelea kutumia soko la Afrika Mashariki kuuza bidhaa zake ambapo magazeti ya HabariLeo na Daily News yameendelea kuuzwa nchini Kenya na Rwanda. Aidha, mtambo mpya wa uchapaji wa kibiashara umewasili na kazi ya kukarabati jengo ambalo mtambo utafungwa ipo kwenye hatua za mwisho. Uzinduzi wa mtambo huo unatarajiwa kufanyika kabla ya mwezi Juni, 2019 na huduma za uchapaji ikiwemo uchapaji wa vitabu, majarida, taarifa, vipeperushi, shajara, kalenda na utengenezaji

wa mabango zitaanza kutolewa.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni imeendelea kuendesha majukwaa ya fursa za biashara na uwekezaji katika Mikoa ya Geita, Lindi na Tabora yaliyohudhuriwa na zaidi ya washiriki 1,600 wakiwemo wawakilishi wa Taasisi za umma na binafsi. Aidha, mawasiliano na baadhi ya Balozi zetu nje ya nchi pamoja na wadau mbalimbali yanafanyika ili kuendesha majukwaa haya nje ya nchi. Balozi za Jumuiya ya Falme za Kiarabu (UAE) na Oman zimeonyesha utayari huo. Katika majukwaa haya TSN hutumia magazeti na vyombo vyake vya kidijiti kuhabarisha na kuhamasisha wananchi na wawekezaji kutumia fursa za biashara na uwekezaji zilizopo na vilevile kupanua biashara ya Kampuni.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi la kujiimarisha ili kukabiliana na ushindani unaotokana na maendeleo ya teknolojia katika Sekta ya uchapaji liliendelea. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuimarisha Kitengo cha Habari Mtandao kwa kukiongezea waandishi na vifaa na kuboresha habari kwa njia ya mtandao kwa kuongeza habari za kijamii na matangazo mubashara kwa matukio mbalimbali. Kutokana na juhudi hizi, Kampuni imeongeza idadi ya wafuatiliaji kwenye Televisheni Mtandao (Daily News Digital) hadi kufikia 47,000 mwezi Machi, 2019 ambapo hakukuwa

na wafuatiliaji kipindi hicho mwaka 2018. Jitihada hizi pamoja na kuanzisha programu tumizi ya kuuza magazeti kwa njia ya mtandao zimeongeza mapato ya Kampuni.

3.2.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni inahusisha kuenzi, kulinda, kuhifadhi na kuweka kumbukumbu za urithi wa utamaduni ikiwa ni pamoja na historia, mila, desturi, sanaa, lugha, maadili na uzalendo.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi la kuhuisha Sera ya Maendeleo ya Utamaduni ya Mwaka 1997 liliendelea kufanyika kwa kukusanya maoni ya Wadau. Aidha, tathmini ya utekelezaji wa Sera hiyo katika kipindi cha miaka 22 ili kubaini mafanikio na changamoto na masuala ya kuzingatiwa katika Sera mpya inafanyika.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** utafiti wa lugha, mila na desturi za makundi makuu manne (4) ya ki-lugha kwa jamii zenye wazungumzaji wachache ulifanyika Wilaya ya Mbulu, Mkoani Manyara. Makabila hayo ni Wabantu (Wanyiramba/ Wanyisanzu); Wanailo (Wadatoga); Wakhoisa (Wahadzabe) na Wakushi (Wairaqw). Aidha, utafiti ulijikita katika kutambua mila na desturi za jamii hizo ikiwemo, ngoma, vyakula na mavazi ya asili pamoja na sherehe za kimila

ili kuweka kumbukumbu kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Vilevile, utafiti wa kina kuhusu mila na desturi za Jamii ya Waluguru na utawala wa Chifu Kingalu Mwanabanzi wa XV, ulifanyika katika Kata ya Kinole, Mkoani Morogoro. Utafiti ulilenga kubaini na kuorodhesha urithi wa utamaduni ikiwamo kujenga makumbusho ya kihistoria katika eneo hilo.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa na takwimu za maeneo ya kihistoria, utamaduni, mila na desturi ulifanyika kwa Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe na Tanga. Uchambuzi umebaini Maeneo 274 yenye kumbukumbu za kihistoria ikiwemo makaburi yenye historia za Machifu, wapigania uhuru na wakoloni wa kiingereza na kijerumani pamoja na historia za mashujaa wa Vita vya Majimaji na chemchemu za maji zilizotumika kwa shughuli za matambiko. Kumbukumbu zote zimehifadhiwa kwa njia ya TEHAMA kwa ajili ya utafiti zaidi na kwa matumizi ya vizazi vya sasa na vijavyo.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi la ubainishaji na uorodheshaji wa takwimu za Maafisa Utamaduni wa Mikoa na Halmashauri zote Tanzania Bara lilifanyika kwa lengo la kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa

Sera ya Utamaduni katika ngazi hizo. Jumla ya Mikoa 24 na Halmashauri za Wilaya 184 zimewasilisha takwimu hizo. Aidha, Kikao Kazi cha Maafisa Utamaduni kilifanyika tarehe 27 - 28 Februari, 2019, Jijini Dodoma kikiwa na Kauli mbiu *"Umoja, Upendo na Kazi, Asili ya Utamaduni Wetu"*. Kikao kiliazimia kuimarisha usimamizi na maendeleo ya Sekta ya Utamaduni.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** katika ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili kitaifa na kimataifa, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imeandaa rasimu ya awali ya Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) na Mwongozo kwa ajili ya nchi zenye uhitaji wa wataalamu wa kufundisha Kiswahili. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Taasisi zinazohusika na lugha ya Kiswahili za BAKITA, BAKIZA, TATAKI na Vyuo Vikuu nchini inaandaa Mwongozo na vitabu kwa ajili ya nchi hizo.

Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki iliratibu tathmini ya maendeleo ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tathmini hiyo ambayo ilifanyika mwezi Juni, 2018 Jijini Arusha, ililenga kupata takwimu sahihi zitakazotumika kupima maendeleo ya lugha ya Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

48. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa wadau wa Sekta ya Utamaduni wakiwemo wasanii wa kazi za sanaa na ubunifu, Wizara ilianza zoezi la kuhuisha Mfuko wa Utamaduni ambapo rasimu ya Andiko la kuhuisha Mfuko iliandaliwa kwa hatua ya kupata maoni ya wadau.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu ni Mratibu wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika yenye jukumu la kubaini, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu kuhusu harakati za ukombozi wa Bara hili. Kumbukumbu hizo ni pamoja na vifaa, maeneo, majengo, nyaraka, mahandaki, maelezo, sare, silaha, magari na kumbukumbu nyingine zilizotumika wakati wa harakati za kulikomboa Bara hili. Aidha, Taifa letu lilipewa jukumu hili na Umoja wa Afrika Mwaka 2011 kutokana na kuwa kiongozi, ngome na kinara wa kuongoza mapambano ya harakati za kulikomboa Bara la Afrika.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki maeneo 94 yaliyotumika wakati wa harakati za ukombozi wa Bara la Afrika yalibainishwa kwa lengo la kukarabatiwa ili yatumike kama vivutio vya utalii wa kiutamaduni na kuhifadhi urithi wa ukombozi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya maeneo 255 yamebainishwa na kuorodheshwa kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. II**. Aidha, vifaa na nyaraka mbalimbali 6,782 kuhusu historia ya ukombozi

wa Bara la Afrika vilibainishwa na kukusanywa kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. III**. Lengo ni kuvihifadhi kwa njia ya kidijiti na kuwekwa katika makumbusho ya historia ya ukombozi wa Afrika itakayojengwa Jijini Dar es Salaam. Aidha, Wizara inaendelea na zoezi la kuandaa Sheria itakayosimamia uhifadhi na uendelezaji wa maeneo yenye historia ya ukombozi wa nchi yetu na Afrika kwa ujumla.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** ukarabati wa jengo lililopo Jijini Dar es Salaam lililokuwa likitumiwa na Kamati ya Ukombozi wa Bara la Afrika kwa takribani miaka 30 umeendelea. Aidha, ikiwa ni hatua ya kutoa elimu kwa umma na ulimwengu kwa ujumla kuhusu harakati za kulikomboa Bara la Afrika, zoezi la kuanzisha tovuti ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika liliendelea kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) ambapo kazi iliyobaki ni kuingiza taarifa mbalimbali. Vilevile, uliandaliwa Mpango wa Kikanda wa Miaka Mitano (5) wa Utekelezaji wa Programu pamoja na Mpango wa Kitaifa wa Miaka Mitano (5) wa utekelezaji wa Programu hiyo ambavyo vimewasilishwa kwa wadau wa ndani na nje ya nchi kwa utekelezaji wa vipaumbele na malengo ya Mipango hiyo.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kujitawala, nchi za ki-Afrika ziliendelea kutumia vitabu vya historia vilivyoandikwa na wale wale

waliotutawala. Hali hii imesababisha michango ya baadhi ya mashujaa wetu wa harakati za ukombozi, kwa makusudi, kutoakisiwa na kutothaminiwa ipasavyo. Mathalan, shujaa Leti Hema wa Wanyaturu, Mwanamama aliyesimama kidete kuzuia utawala wa Kijerumani kwa zaidi ya miaka mitatu (3) kwa kutumia makundi ya nyuki yaliyouma wazungu tu na kuwazuia Wajerumani wasikaribie kilima cha Ng'ongo Ipembe na maeneo yaliyokizunguka (sasa Singida Mjini). Hata alipouawa na Wajerumani baada ya kusalitiwa, wakoloni hao hawakuridhika, waliamua kukata kichwa chake na kukipeleka Ujerumani kwa uchunguzi wa kina ili kubaini kama alikuwa na uwezo maalumu wa kibiolojia wa kufundisha wadudu wenye ubongo mdogo sana kama nyuki, kuwashambulia wazungu tu na muujiza aliowaonesha alipokutana nao kwa mazungumzo yaliyovunjika wa kukaa juu ya ncha kali ya mkuki badala ya kigoda cha kawaida.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** shujaa huyu pamoja na Mashujaa wengine wengi wa Harakati za Ukombozi kama vile Mtemi Isike wa Tabora aliyepigana na Wajerumani kwa zaidi ya miaka minne (4) na hatimaye kuzidiwa nguvu na kujinyonga na Nduna Mkomanile wa Wangoni, mwana mama mwingine aliyepambana kishupavu dhidi ya Wajerumani na kuuawa, hawajaandikwa wala mchango wao kuthaminiwa katika historia ya Nchi yetu

iliyoandikwa na wazungu. Mbali na kufufua kampeni ya kurejesha fuvu la shujaa Leti na mashujaa wengine, Wizara itasimamia kampeni ya kuhimiza watafiti wetu kuandika upya historia ya Ukombozi wa Nchi yetu na Afrika kwa ujumla ili kuwezesha wanafunzi na vijana wetu kusoma historia yetu ambayo haijapotoshwa kwa makusudi na hivyo kuwajengea moyo wa uzalendo, utaifa, mshikamano, umoja na upendo.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe pongezi nyingi kwa wadau wa Programu hii wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, ambao wanaunga mkono juhudi za kuhifadhi historia ya ukombozi wa Bara la Afrika kwa kubuni miradi mbalimbali hususan ujenzi wa makumbusho katika maeneo yaliyotumiwa na Wapigania Uhuru kutoka Nchi za Kusini mwa Afrika. Nianze na wewe Mheshimiwa Spika na Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kwa wazo la kuanzisha Mpango wa kujenga *Kongwa Freedom Fighters Memorial Park.* Aidha, nampongeza pia Mbunge wa Tunduru-Kaskazini Mheshimiwa Mhandisi Ramo Matala Makani kwa jitihada za kuendeleza eneo lililotumiwa na Wapigania Uhuru wa FRELIMO kutoka Msumbiji kwa kuandaa maadhimisho ya Siku ya Tunduru-Masonya ***(Tunduru-Masonya Day)*** yatakayofanyika mwezi Julai 2019. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wana maeneo yaliyotumiwa na Wapigania Uhuru

katika Majimbo yao, waendelee kubuni miradi mbalimbali ya kuyaendeleza na kuyahifadhi kwa ajili ya kukuza utalii wa kiukombozi na wa kiutamaduni.

3.2.2.1 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)

55. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ni pamoja na kuratibu na kusimamia matumizi na maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini na kufuatilia maendeleo yake nje ya nchi.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya vipindi 564 vya redio na televisheni vilivyolenga kuelimisha umma kuhusu lugha ya Kiswahili viliandaliwa. Vipindi vilijikita katika matumizi fasaha na sanifu ya lugha, stara ya lugha, historia ya lugha, fursa za lugha ya Kiswahili, uundaji wa maneno katika lugha na masuala mengine yanayohusiana na sarufi na fasihi. Miongoni mwa vipindi hivyo ni: Kumepambazuka Kiswahili 34, Kiswahili Mtaani 10 na Ufafanuzi wa Msamiati wa Kiswahili na Matumizi yake 520.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya vitabu 45 vya kiada na ziada vilipitiwa na kupewa ithibati kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. IV**. Aidha, tafsiri ya nyaraka 1,293 za Mashirika, Kampuni na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali pamoja na za watu binafsi zilitolewa. Vilevile, huduma ya tafsiri na ukalimani ilitolewa

wakati wa Mkutano wa Bunge la Afrika Jijini Kigali - Rwanda tarehe 18 Oktoba - 3 Novemba, 2018. Pia, utomeshaji wa vidahizo 10,000 vya Kamusi ya Kiswahili – Kiswahili kwa Shule za Msingi ulikamilika na uhariri wa mwisho unafanyika kabla ya Kamusi hiyo kuchapwa Desemba, 2019. Vilevile, makala 11 za Jarida la Lugha Yetu zinazohusiana na historia, sarufi na fasihi ya Kiswahili zimeandaliwa na zoezi la uhariri lipo katika hatua za mwisho.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** matini za maneno 1,500,000 zilizotokana na vitabu vya waandishi nguli wa riwaya na siasa ziliandaliwa na kupakiwa kwenye seva ya kongoo la Kiswahili. Vitabu hivyo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. V**. Aidha, istilahi 300 za nyanja mbalimbali kwa ajili ya usanifishaji zimeandaliwa. Vilevile, vituo vinne (4) vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni vya Dar es Salaam Language School, Peace Corps Tanzania, Learn Swahili Language Centre na MS- TCDC Arusha vimetambuliwa na kupewa vyeti vya utambuzi.

59. ***Mheshimiwa Spika***, zoezi la kusajili wataalamu wa Kiswahili katika kanzidata ya watalaamu hao tuliyoianzisha liliendelea ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya watalaamu 624 (Me: 284 na Ke: 340) wamesajiliwa. Aidha, mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni yametolewa kwa wataalamu hao katika

Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na Mwanza na mipango ya kufikia Mikoa mingine inaendelea. Natoa wito kwa wataalamu wa lugha ya Kiswahili kote nchini kujisajili katika kanzidata hii ili wanufaike na fursa zake ikiwemo ukalimani na kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni. Hivi sasa tuna maombi kutoka nchi nyingi za ndani na nje ya Bara la Afrika yanayohitaji walimu wa Kiswahili kwa ngazi mbalimbali za masomo. Kama nilivyoeleza awali, kwa sasa tunakamilisha Mwongozo wa ufundishaji wa Kiswahili kwa ngazi mbalimbali na zoezi hili ni shirikishi. Wizara yangu; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (waratibu); Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Vyuo Vikuu na Taasisi za Maendeleo ya Kiswahili Tanzania Bara na Zanzibar tunahusika. Aidha, Semina kuhusu matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili kulingana na maadili ya jamii na iksadi ya lugha hiyo ilifanyika kwa watangazaji wa E-FM (30), Mlimani Redio na Televisheni (39), Channel Ten (21) Times FM (21), TBC Taifa (23) na TBC 1 (27). Utaratibu wa kuwafikia watangazaji wa redio na televisheni nyingine unaendelea kutekelezwa.

3.2.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA

60. ***Mheshimiwa Spika***, majukumu ya Sekta hii ni pamoja na kusimamia maendeleo ya shughuli za sanaa, filamu na ubunifu.

61. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Septemba, 2019 Tanzania itakuwa mwenyeji wa Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) linalohusu kuhifadhi, kulinda, kuendeleza na kutangaza urithi wa utamaduni; sanaa na ubunifu pamoja na shughuli za filamu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Maandalizi yanafanyika kupitia Kamati ya Kitaifa na Kamati Ndogondogo za maandalizi. Aidha, kikao cha kwanza cha Kikanda cha Jumuiya ya Afrika Mashariki kimefanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Machi, 2019. Kaulimbiu ya Tamasha ni: *Uanuai wa Kiutamaduni: Msingi wa Utangamano wa Kikanda, Maendeleo ya Kiuchumi na Kushamiri kwa Utalii* (*Cultural Diversity; A Key Driver to Regional Integration, Economic Growth and Promotion of Tourism).*

62. ***Mheshimiwa Spika***, Tamasha hili litahusisha shughuli mbalimbali yakiwemo matembezi ya shamrashamra za ngoma (kanivali) na maleba/mavazi yanayotoa fursa kwa kila nchi mwanachama kuonesha utajiri wake wa utamaduni; maonesho na biashara ya bidhaa za kitamaduni na sanaa; kongamano na warsha kuhusu utamaduni; maonesho na mashindano ya filamu; michezo ya jadi na watoto na maonesho na soko la vyakula vya asili, mavazi na ulimbwende. Zaidi ya washiriki 1,200 kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, washiriki na wanunuzi zaidi ya 100,000 (baadhi kutoka nje ya Afrika) wanatarajiwa kushiriki.

Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha wadau mbalimbali wakiwemo wajasiriamali na wanautamaduni katika maeneo yao kushiriki katika Tamasha hili ili kutangaza na kuuza kazi zao pamoja na kuanzisha mitandao ya kibiashara itakayoimarisha masoko ya kazi zao ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

63. ***Mheshimiwa Spika***, kampeni ya Uzalendo na Utaifa iliyobeba Kauli Mbiu: ***"Kiswahili Utashi Wetu, Uhai Wetu"*** ikiwa na lengo la kuenzi na kusisitiza matumizi sahihi na fasaha ya lugha adhimu ya Kiswahili pamoja na kuhamasisha uzalendo, ilifanyika na kufikia kilele tarehe 08 Desemba, 2018 Jijini Dodoma. Kampeni hii ambayo hufanyika kila mwaka kwa lengo la kuhamasisha uzalendo na utaifa, iliambatana na Mdahalo tarehe 14 Oktoba, 2018 siku ya kumbukizi ya Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere. Aidha, midahalo juu ya uzalendo na utaifa kwa wanafunzi wa baadhi ya Shule za Sekondari za Wilayani Bahi na Chamwino Mkoani Dodoma imefanyika.

64. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kushirikiana na wadau, Wizara iliratibu na kushiriki katika matamasha na matukio mbalimbali ya Sanaa. Matamasha hayo ni Tamasha la 37 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, Tamasha la 10 la muziki wa Cigogo lililofanyika mwezi Julai, 2018 Mkoani Dodoma na uzinduzi wa

shindano la saba la ulimbwende la Dunia la Wanahabari *(Miss Journalism World 2018)* lililofanyika mwezi Agosti, 2018 Mkoani Arusha.

3.2.3.1 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)

65. ***Mheshimiwa Spika***, majukumu ya Baraza hili ni kuratibu na kusimamia Sekta ya Sanaa nchini.

66. ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua ya kurahisisha upatikanaji wa huduma zake, Baraza limegawa shughuli za uratibu wa utoaji wa huduma katika Kanda sita (6) za Nyanda za Juu Kusini, Kati, Kaskazini, Ziwa, Pwani na Kanda Maalum ya Dar es Salaam ambapo huduma hutolewa moja kwa moja kwa wadau. Aidha, ili kuimarisha utoaji wa taarifa kwa wadau, Baraza liliboresha tovuti yake www.basata.go.tz, wavuti; basatatz.blogspot.com na mitandao ya kijamii ya *facebook* (www.facebook.com/basatatz) na *twitter* (www.basata.com/basatatanzania). Vilevile, ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Maonesho uliendelea kwa kuweka milango na madirisha na kazi zilizosalia ni uwekaji wa miundombinu ya jukwaa, sauti, taa maalum, viti vya watazamaji, viyoyozi, marumaru na sakafu ya mbao. Matarajio yetu ni kukamilisha kazi hii ndani ya mwaka ujao wa fedha.

67. ***Mheshimiwa Spika***, maudhui ya kazi za muziki 342 yamehakikiwa na kupewa idhini ya kutumika. Midahalo 36 ya Jukwaa la Sanaa iliyoshirikisha wasanii na wadau 3,170

ilifanyika kwa lengo la kutoa elimu ya masuala ya sanaa ikiwa ni pamoja na maadili. Vilevile, kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi mbalimbali ikiwemo COSOTA na Bodi ya Filamu operesheni za kukagua kazi za sanaa zisizo rasmi (kazi zisizo na stika za Mamlaka ya Mapato Tanzania) pamoja na ufuatiliaji wa mitambo na vifaa vinavyotumika kudurufu kazi za Sanaa bila ridhaa ya wahusika zilifanyika.

68. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliendelea kuchukua hatua mbalimbali ya kuwajengea uwezo wasanii na wajasiriamali wa kazi za Sanaa za Ufundi ili waweze kuzalisha kazi bora zinazoendana na mahitaji ya soko. Katika kutekeleza azma hii, yameendeshwa mafunzo ya siku nne (4) kuhusu matumizi ya mitandao katika kutangaza na kuuza kazi za sanaa Mkoani Arusha kuanzia tarehe 17 – 20 Desemba, 2018. Jumla ya viongozi wa vyama na vikundi vya wasanii na wadau wa Sanaa 60 (Ke: 27, Me: 33) walishiriki.

69. ***Mheshimiwa Spika***, kupitia Mradi wa Utambuzi wa Wasanii wa sanaa za ufundi Tanzania (TACIP), takribani wasanii wa Sanaa za Ufundi wapatao 6,000 kutoka Halmashauri za Wilaya ya Kinondoni na Ubungo, Mkoani Dar es Salaam wametambuliwa. Lengo ni kuwa na kanzidata mahususi ya wanasanaa za ufundi itakayoruhusu mageuzi makubwa ya maendeleo ya tasnia hii kiweledi na kimasoko

ndani na nje ya nchi kwa kutumia TEHAMA ambapo kila mwanasanaa atakuwa na utambulisho wake na wa kazi zake kielektroniki. Vilevile, Baraza litaendesha mafunzo ya sanaa kwa watoto katika Mkoa wa Mwanza kuanzia tarehe 15 hadi 18 Aprili, 2019. Mafunzo haya yanahusisha wanafunzi 100 na walimu watano (5) kutoka katika shule za msingi tano (5) za Mkoani Mwanza. Pia, usajili na utoaji wa vibali vya kuendesha shughuli za sanaa kwa wasanii na wadau wa sanaa wapato 1,084 Tanzania Bara umefanyika.

70. ***Mheshimiwa Spika***, ikiwa ni hatua ya kutoa elimu na taarifa mbalimbali za Sekta ya Sanaa kwa wadau, Baraza lilishiriki katika Maonesho ya Biashara ya Sabasaba ya mwaka 2018 ambapo wasanii 117 walipata fursa ya kutangaza na kuuza bidhaa zao. Vilevile, ushauri kwa wasanii na wadau wa sanaa 2,638 kutoka maeneo mbalimbali nchini katika masuala ya masoko ya kazi za sanaa, uendeshaji wa matukio, utafutaji fedha kwa vikundi na taasisi pamoja na masuala ya usajili na vibali ulitolewa. Pia, tathmini ya matukio ya sanaa yanayoendeshwa na wadau ikiwa ni pamoja na *Tigo Fiesta, Bongo Star Search, Miss Tanzania na Stand Up Comedy* ilifanyika na kumbukumbu za wasanii mahiri kwa matumizi ya kizazi cha sasa na kijacho zilikusanywa na kuhifadhiwa.

3.2.3.2 Bodi ya Filamu Tanzania

71. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Filamu Tanzania ilianzishwa kwa Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya 1976 na majukumu yake ni pamoja na kusimamia utayarishaji wa picha jongevu na michezo ya kuigiza; kuhakiki na kuweka madaraja katika picha jongevu na michezo ya kuigiza; kusimamia usambazaji na uoneshaji wa kazi hizo na kutoa ithibati kwa miundombinu, makampuni na wadau wa filamu na michezo ya kuigiza.

72. ***Mheshimiwa Spika***, miswada 124 ya filamu ndefu na filamu za makala zilizowasilishwa ilipitiwa, kuchambuliwa na kutolewa maoni. Jumla ya vibali 121 vya utayarishaji wa picha jongevu vilitolewa ambapo 22 vilitolewa kwa waombaji kutoka ndani ya nchi na 99 kutoka nje ya nchi. Aidha, vibali kwa maombi matatu (3) yaliyosalia vitatolewa baada ya taratibu kukamilika. Ili kuhakikisha sheria zinazingatiwa ipasavyo katika upigaji picha za filamu, usimamizi uliimarishwa kwa waombaji kutoka nje ya nchi ikiwemo Australia, Canada, China, Japan, Kenya, Marekani, Ubelgiji na Uingereza waliokuja nchini kutengeneza filamu zenye maudhui ya masuala ya kiutamaduni na kijamii.

Kielelezo Na. 4: Vibali Vilivyotolewa kwa Watayarishaji wa Filamu Kutoka Ndani na Nje ya Nchi Mwaka 2018/19



Aidha, **Kimbatisho Na VI** ni idadi ya vibali vya utayarishaji wa kazi za filamu na picha jongevu vilivyotolewa mwaka 2013/14 hadi 2018/19.

73. ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya filamu (DVD) 961 zilihakikiwa na kupangiwa madaraja sawa na asilimia 120 ya lengo la filamu 800. Kati ya filamu zilizohakikiwa, 821 ni za Kitanzania, na 140 ni kutoka nje ya nchi zikijumuisha filamu zilizohakikiwa katika Majumba ya Sinema. Aidha, kati ya filamu zilizowasilishwa, filamu sita (6) za Kitanzania zenye majina *Siri ya Majini, Mzalendo Halisi, Bunge la Bongo*, "*Ndoto za Kitaa*", *Mdoo wa Kitaa, Outh Bound Obssession* zilitolewa ushauri wa kitaalamu na Bodi na kuelekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuboresha kasoro za kiufundi kuimarisha

ubora wa kazi hizo pamoja na kurekebisha kasoro za maudhui ambazo zipo kinyume na sheria, kanuni na taratibu. Vilevile, filamu iitwayo "*Ek-ladki-ko-dekha to aisa laga*" yenye asili ya India haikupewa kibali cha kusambazwa nchini kutokana na maudhui yanayoshawishi mapenzi ya jinsi moja (Usagaji) kinyume cha sheria za nchi.

Kiambatisho Na. VII ni filamu za ndani na nje ya nchi zilizohakikiwa na kupewa vibali mwaka 2013/14 - 2018/19. Aidha, Kielelezo Na. 5 ni Filamu za Kitanzania na za Nje ya Nchi zilizohakikiwa na Bodi ya Filamu Tanzania 2018/19.

Kielelezo Na.5: Kazi za Filamu za Kitanzania na za Nje ya Nchi Zilizohakikiwa na Bodi ya Filamu Tanzania Mwaka 2018/19



74. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya maeneo 317 yasiyokuwa rasmi ya kusambazia na kuoneshea picha jongevu yalibainishwa katika Mikoa ya Manyara, Songwe na Tanga kwa lengo la kuyarasimisha na kupanua wigo wa soko la bidhaa za filamu nchini. Maeneo hayo ni vibanda 44 vya kuoneshea filamu, maktaba 237 za kusambazia filamu na studio 36. Aidha, leseni tisa (9) kwa ajili ya uendeshaji wa majumba ya sinema ikiwemo ya 12D Sinema (gari la sinema), 15 kwa ajili ya usambazaji wa kazi za filamu, 15 za shughuli za filamu (utayarishaji, uendeshaji wa Kampuni, uoneshaji wa filamu na Tamasha la Filamu) na mbili (2) kwa ajili ya uendeshaji wa Studio zilitolewa.

Vilevile, ulifanyika ukaguzi wa majumba ya sinema ya Century Cinemax (Mlimani City, Aura Mall, Dar Free Market, Mkuki House), City Mall Cinemax, Cineplex Cinema na City Mall Cinema (Dar es Salaam), New Majestic (Tanga), Mysterios Cinematics (Mwanza), Regalz Cinema (Njiro na Burka/Majengo – Arusha) na kuridhika na uendeshaji wake. Kutokana na ukaguzi huo majumba rasmi ya uoneshaji wa picha jongevu Tanzania yamefikia 11 ambapo 7 yapo Dar es Salaam, 1 - Tanga, 2 - Arusha, na 1 - Mwanza,

75. ***Mheshimiwa Spika,*** semina ya kujenga uwezo na kuimarisha weledi kwa viongozi wa Shirikisho la Filamu Tanzania (TAFF),

Bodi ya Shirikisho hilo na Vyama vyake 11 vinavyojishughulisha na masuala ya filamu ilitolewa. Semina hiyo ilifanyika tarehe 17-18 Desemba, 2018 Mkoani Morogoro na ilijikita katika kuimarisha mifumo ya vyombo hivyo na kuweka mikakati ya kujiimarisha.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuhakikisha wadau wa filamu wanazalisha kazi bora kwa kuzingatia weledi, yaliendeshwa mafunzo ya kuwajengea uwezo katika Mikoa ya Manyara (wadau 104), Songwe (wadau 215) na Tanga (wadau 260). Mafunzo yalijikita katika maeneo ya uandishi wa miswada ya filamu; kujitangaza, kutangaza biashara na usimamizi; uongozaji wa filamu, taaluma ya upigaji picha katika uzalishaji wa filamu bora; matumizi ya mtandao katika Sekta ya Filamu; umuhimu wa filamu katika ukuzaji wa Lugha ya Kiswahili; uhusiano kati ya mtunzi, mwongozaji na mwigizaji; elimu kuhusu rushwa; Mikataba na Makubaliano, Hakimiliki na Hakishiriki na Wajibu na Majukumu ya Bodi ya Filamu katika kukuza Sekta ya Filamu nchini. Mafunzo haya yataendelea katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Kigoma, na Ruvuma.

Aidha, Bodi iliendesha operesheni za kawaida 20 katika maeneo ya Kariakoo, Gongo la Mboto, Segerea, Manzese, Kigogo (Dar es Salaam), Tunduma, Vwawa na Mlowo (Songwe) ambapo jumla ya filamu 28 zilibainika kuingizwa

sokoni kinyume cha sheria. Hatua za kisheria zimeendelea kuchukuliwa kwa wahusika.

77. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia tangazo la Wizara la kupitia upya mikataba mibovu waliyoingia baadhi ya wasanii na hivyo kuathiri kipato chao, Kamati ya kupitia Mikataba ya Wadau wa Filamu iliundwa na kuchambua Mikataba 11 iliyowasilishwa. Baadhi ya Kampuni zimethibitisha kuwalipa wahusika viwango vya kuridhisha na zingine zimeingia kwenye makubaliano maalumu na Kamati kuongeza malipo kwa viwango mbalimbali. Kwa mfano:

a) Kampuni za Pan-Africa Enterprises Ltd na Ivori Iringa zimeshaingiza kwenye Akaunti maalumu Shilingi 30,000,000 kwa kazi alizotekeleza marehemu Amri Athumani (King Majuto) kimkataba. Aidha, Kampuni ya Azam – SSB imeandaa malipo ya ziada ya Shilingi 20,000,000 na Kampuni ya Tanfoam ya Arusha Shilingi 15,000,000 ambayo yatawasilishwa kwa msimamizi wa mirathi ya marehemu King Majuto. Vilevile, baadhi ya kampuni ikiwemo Neelkanth Salt Ltd, zimejiwekea utaratibu wa kuridhisha wa mawasiliano ya moja kwa moja na familia ya King Majuto.

b) Kampuni ya Steps Entertainment imekwishamkabidhi mama wa marehemu Steven Kanumba malipo ya ziada ya Shilingi 15,000,000 na Kampuni hiyo

imeahidi kushirikiana naye kuandaa filamu ya maisha ya mwanawe.

c) Kampuni ya Steps Entertainment tayari imemlipa msanii Sikujuwa Mbwewe Shilingi 6,750,000 kutokana na kusambazwa kwa filamu yake ijulikanayo kwa jina la "Utu Wangu" bila ya ridhaa yake na filamu hiyo amerejeshewa.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** orodha ni ndefu ikizingatiwa kwamba hatua zingine za kuondoa manung'uniko katika tasnia zinafanyika kupitia Chama cha Hatimiliki Tanzania (COSOTA) ambacho kiko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Hata hiyo, kinafanya kazi kwa karibu na taasisi zote za sanaa za Wizara yangu. Migogoro iliyotatuliwa na COSOTA ni pamoja na Akim Igembe kumlipa Anna Joseph Shilingi 6,000,000 kwa kuwahisha sokoni filamu yake "NAINA" bila ruhusa yake; Murchy Ben International imemlipa Jenista Raymond Mao Dola za Marekani 1,500 kwa kuingiza mtandaoni filamu yake "PERFECT WHITE" bila kibali chake na mwanamuziki Peter Msechu ameilipa bendi kongwe ya muziki wa dansi hapa nchini, Atomic Jazz Band ya Tanga, Shilingi 1,000,000 kwa kukarabati na kuimba wimbo wao wa "TANZANIA YETU" bila ruhusa yao. Aidha, Kamati ya Kupitia Mikataba bado haijafikia maridhiano na kampuni saba (7) zifuatazo:

a) Kwa kazi za Marehemu King Majuto: Kampuni za Freedom Film Production, Afsar Furniture, Sterling Surfactants Ltd, Al-Riyamy Production, Al-Abdi's Entertainments na Tigo;

b) Kazi za Marehemu Steven Kanumba: Kampuni ya Startimes; na

c) Kwa kazi ya Wastara Juma: Kampuni ya KZG Service Ltd.

Nazihimiza kampuni hizi zifikie makubaliano na Kamati mapema iwezekanavyo bila kulazimika kuzipeleka mahakamani. Nawahimiza vilevile wadau wote wa sanaa kuhakikisha hawaingii mikataba yoyote bila ushauri wa kisheria. Nitumie fursa hii, kuwashukuru na kuwapongeza wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kwa kujitolea na kwa uadilifu mkubwa.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya Tamasha na Tuzo za Kimataifa la Serengeti *(Serengeti International Festival and Awards*) yameendelea kwa kukamilisha Andiko la Tamasha, kukutana na wadau wa udhamini na kukamilisha logo na ubunifu wa tuzo (trophy). Tamasha hili litazinduliwa mwezi Mei, 2019 na litaendeshwa sambamba na Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo usiku wa tuzo unatarajiwa kuwa tarehe 27 Septemba, 2019.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Bodi ya Filamu Tanzania imeendelea kuwawezesha wadau wa filamu kushiriki katika tuzo na matamasha mbalimbali ndani na nje ya nchi kama vile Udada Film Festival (Kenya), *Urban Film 14th Edition East Africa* (Kenya), Kalasha (Kenya), *Ethiopian Film Festival* (Ethiopia), 38th *Annual Minneapolis St.Paul International Film Festival* (Marekani), *Cannes* (Ufaransa), *Maisha Magic* (Tanzania/Kenya), Tuzo za Filamu za Korea na *Egypt Animation Film Festival* (Misri), *Sinema Zetu Film Festival* na *Zanzibar International Film Festival (ZIFF*) ili kujitangaza na kupanua masoko ya kazi zao. Aidha, kumekuwa na ongezeko la kutumia mifumo mbalimbali ya masoko ya bidhaa za filamu ikiwemo *Apps*, Online TV na televisheni. **Kiambatisho Na. VIII** ni Tuzo mbalimbali za filamu zilizotolewa kwa wanatasnia wa kazi za filamu mwaka 2013/14 - 2018/19.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha masoko ya mazao ya filamu Bodi kwa kushirikiana na Kampuni ya *Clouds Plus Production* na Chuo Kikuu cha Jijini Dar es Salaam iliandaa na kuratibu Jukwaa la Wasambazaji, Watangazaji na Watayarishaji wa maudhui ya filamu lililofanyika Dar es Salaam. Katika jukwaa hilo Kampuni ya *Aret* na DM zote kutoka nchini Italia zilishiriki kwa kufanya maonesho ya kazi na huduma zake pamoja na kubadilishana uzoefu na wadau mbalimbali katika sekta ya filamu nchini.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi la uandaaji wa Sera ya Filamu liliendelea ambapo rasimu ya kwanza ya Sera iliwasilishwa Serikalini na kutolewa maoni ya kuiboresha. Rasimu iliyoboreshwa itawasilishwa tena kwa hatua za uamuzi. Aidha, rasimu ya Kanuni za Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (Vituo, Maktaba na Maeneo ya Kuonyesha na Kusambazia Picha Jongevu isipokuwa Majumba ya Sinema) za mwaka 2019 imekamilika kwa hatua za kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. Kanuni hizi zitasaidia sana kudhibiti uoneshaji wa filamu kiholela bila kuzingatia maadili ya nchi.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Jumba Changamani la Uzalishaji wa Filamu lenye ukubwa wa mita za mraba 46,080 limepatikana Wilayani Chamwino, Jijini Dodoma. Hatua inayofuata ni kufanya Tathmini ya Mazingira na kuandaa michoro.

3.2.3.3 Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)

84. ***Mheshimiwa Spika***, jukumu la TaSUBa ni kutoa mafunzo ya Sanaa na Utamaduni katika ngazi ya Cheti au Astashahada na Stashahada pamoja na mafunzo ya muda mfupi ya kuwajengea uwezo wasanii.

85. ***Mheshimiwa Spika***, mafunzo ya Stashahada, Cheti na kozi fupi katika maeneo ya Sanaa za Maonesho, Sanaa za Ufundi, Filamu na

Televisheni, na Ubunifu wa Muziki yameendelea kutolewa. Jumla ya wanachuo 251 (Wanaume 199 na Wanawake 52) wamedahiliwa. Aidha, jumla ya wanachuo 118 (Wanaume 96 na Wanawake 22) walihitimu mafunzo ya kozi ngazi ya Astahashada na Stashahada kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. IX**. Jumla ya wanachuo 105 (Wanaume 90 na Wanawake 15) walihitimu mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, Mitaala ya kozi zifuatazo imehuishwa ili kuendana na mahitaji kulingana na mabadiliko yaliyotokea katika eneo la sanaa na utamaduni:-

a) Kozi za Astashahada (Certificate) mwaka mmoja (1),
   (i) Sanaa za Maonesho na Ufundi *(Certificate in Performing and Visual Arts)*
   (ii) Teknolojia ya Muziki na Sauti *(Certificate in Music and Sound Technology)*
   (iii) Picha Jongevu na Uzalishaji wa Vipindi vya televisheni (*Certificate in Film and TV Production)*

b) Kozi za Stashahada (Diploma) miaka 2, ina kozi zifuatazo (NTA 5 & 6):
   (i) Sanaa za Maonesho na Ufundi *(Diploma in Performing and Visual Arts)*
   (ii) Teknoloji*a* ya Muziki na Sauti *(Diploma in Music and Sound Technology)*
   (iii) Picha Jongevu na Uzalishaji wa Vipindi vya televisheni *(Diploma in Film and Television Production)*

86. ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuwezesha wasanii wa kike kupata mafunzo ya utamaduni na sanaa ili kuimarisha weledi na ubora wa kazi zao, TaSUBa imetoa ufadhili wa ada ya masomo kwa wanachuo wa kike 10 kwa Mwaka wa Masomo 2018/19. Aidha, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Bodi ya Filamu zimetoa ufadhili wa gharama za malazi kwa wanachuo hao.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni la Bagamoyo lenye malengo ya kupima kiwango cha maendeleo ya usanii na utamaduni, kuandaa na kutoa fursa kwa wasanii na kujadili mada mbalimbali; kuhamisha au kurithisha utamaduni na thamani yake kwa vizazi vijavyo lilifanyika mwezi Oktoba, 2018 Mjini Bagamoyo. Jumla ya vikundi vya sanaa 89 vilishiriki ambapo 84 vilitoka ndani ya nchi na vitano (5) vilitoka nchi za Kenya (2), Zambia (1), Finland (1) na Ujerumani (1). Maandalizi ya Tamasha la 38 linalotegemewa kufanyika kuanzia tarehe 19 - 26 Oktoba, 2019 yameanza.

3.2.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

88. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Sekta hii ni kuratibu na kusimamia maendeleo ya michezo nchini ikiwa ni pamoja na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika michezo; kuwezesha upatikanaji wa miundombinu, wataalamu na

vifaa vya michezo na kuhakikisha timu na wachezaji wanafanya vizuri katika mashindano na michezo mbalimbali ya kimataifa.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi la kuhuisha Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 linaendelea ambapo rasimu ya marekebisho ya Sera ipo katika hatua za kujadiliwa na kuidhinishwa na Serikali. Aidha, maandalizi ya Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Vijana Wenye Umri chini ya Miaka 17 (AFCON-U17) yanayofanyika nchini tarehe 14 - 28 Aprili, 2019 yaliendelea kufanyika. Ukarabati wa miundombinu ya Viwanja vya Taifa na Uhuru vitakavyotumika katika mashindano hayo umefanyika ikiwemo kujenga Paa la Watu Maalumu (VVIP), kurekebisha eneo maalumu la wanahabari, kukarabati vyumba vya wachezaji vya kubadilishia nguo katika Uwanja wa Taifa na kuweka nyasi mpya za bandia Uwanja wa Uhuru. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa Uwanja wa Michezo Mkoani Dodoma yameendelea kwa kushirikiana na Kamati Maalumu iliyoundwa na Rais. Kazi zilizofanyika ni pamoja na upembuzi yakinifu, tathmini ya mazingira, maandalizi ya mchoro wa uwanja, *"geotechnical Survey"* na "*topographical survey".* Vilevile, ujenzi wa uwanja wa *Baseball* na *Softball* kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)* ulikamilika na kuzinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 6 Desemba, 2018.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma ya kinga na tiba imetolewa katika matukio mbalimbali ya Michezo katika Uwanja wa Taifa na Uhuru. Aidha, wataalamu wa meshiriki kutoa elimu kwa wana michezo katika mafunzo yaliyofanyika Wilayani Mpwapwa (Dodoma), Kwimba (Mwanza) na Iringa Mjini (Iringa). yaliyofanyika Wilayani Mpwapwa, Kwimba Mkoani Mwanza na Iringa Mjini. Vilevile, kazi ya kuchimba kisima cha maji safi, kujenga miundombinu yake pamoja na kukarabati Viwanja vya Michezo vya Netiboli, Kikapu, Mikono na Wavu katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya zilianza na zinatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2018/19.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimeendelea kutoa mafunzo ya michezo ya muda mrefu ambapo idadi ya wanafunzi waliodahiliwa mwaka 2018 ilifika 141 (wanaume 110 na wanawake 31) ikilinganishwa na wanafunzi 125 (wanaume 94 na wanawake 31) waliodahiliwa mwaka 2017. **Kiambatisho Na. X** ni mwenendo wa usajili wa wanafunzi katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya mwaka 2010-2018. Ongezeko hili linatokana na Chuo kupatiwa ithibati na NACTE na hivyo wanafunzi kudahiliwa kadri ya maombi na vigezo vya mamlaka hiyo. Aidha, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya michezo ya muda mfupi ambapo jumla ya washiriki 220 wamepatiwa mafunzo katika

Mikoa ya Dodoma (138), Iringa (48) na Mwanza (34). **Kielelezo Na. 6** ni idadi ya wanafunzi waliosajiliwa katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya mwaka 2013-2018.

Kielelezo Na.6: Wanafunzi Waliosajiliwa katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya Mwaka 2013-2018



92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Taifa letu limepata mafanikio makubwa katika michezo mbalimbali kama ifuatavyo:-

a) Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu *(Taifa Stars)* imefuzu kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Barani Afrika (AFCON) nchini Misri, mwezi Juni, 2019 baada ya kushindwa kufuzu kuingia kwenye fainali hizo kwa miaka 39;

b) Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Vijana chini ya Umri wa Miaka 17 *(Serengeti Boys)* imefuzu katika Mashindano ya Afrika ya Mpira wa Miguu kwa Vijana Wenye Umri chini ya Miaka 17 (AFCON-U17) yatakayofanyika nchini mwezi Aprili, 2019. Pia, timu hii imechukua Ubingwa wa Mashindano Maalumu ya Vijana yaliyofanyika nchini Rwanda mwezi Aprili, 2019 ambayo yalishirikisha timu za Cameroon, Rwanda na Tanzania baada ya timu hiyo kuchukua makombe ya CECAFA na COSAFA mwaka jana;

c) Timu ya Riadha iliyoshiriki Mashindano ya *Nagai City Marathon* yaliyofanyika nchini Japan mwezi Oktoba, 2018 ilishinda Medali 7 (Dhahabu 4, Shaba 2, Fedha 1);

d) Bi. Madina Iddi wa Arusha aliibuka mchezaji bora wa kike Barani Afrika katika mashindano ya Gofu ya Wanawake ya Afrika yaliyofanyika mwezi Agosti, 2018 nchini Ghana;

e) Timu ya Olimpiki Maalum *(Special Olympics)* ilishinda jumla ya Medali 15 katika mashindano ya Riadha na Mpira wa Wavu yaliyofanyika Abu Dhabi, Falme za Kiarabu mwezi Machi, 2019. Kati ya Medali hizo Dhahabu ni 12, Fedha moja (1) na Shaba mbili (2);

f) Timu ya Wanawake ya Mpira wa Miguu *(Kilimanjaro Queens)* ilishinda mashindano ya CECAFA yaliyofanyika mwezi Julai, 2018 Kigali, Rwanda kwa mara ya pili mfululizo. Aidha, timu hiyo iliibuka bingwa wa Mashindano ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Jijini Bujumbura Burundi mwezi Agosti, 2018.

g) Kufuatia mabadiliko makubwa yaliyosimamiwa na Wizara katika ngumi za kulipwa nchini, Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania imeundwa. Chombo hiki kipya cha kusimamia mchezo huo kimeweza katika muda mfupi kuleta mafanikio makubwa katika ndondi za kulipwa kama ifuatavyo:

   i. Fadhili Majiha alimtwanga Rofhiwa Nemushungwa wa Afrika Kusini tarehe 20 Julai, 2018 na kuchukua Mkanda wa WBA Pan Africa Bantam Weight, mchezo uliofanyika Geuteng, Afrika ya Kusini;
   ii. Hassan Mwakinyo alimpiga bingwa wa Uingereza wa uzito wa Super Welter, Sam Eggington kwa TKO katika mzunguko wa pili tarehe 8 Septemba, 2018, Birmingham, Uingereza;
   iii. Twaha Kassim Rubaha a.k.a Twaha Kiduku alimchapa Shariff Kassongo wa DRC na kutwaa mkanda wa UBO Africa Super Welterweight katika

mchezo uliofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 29 Septemba, 2018.

iv. Bruno Melchiory a.k.a Vifuaviwili alimnyuka Joshua English wa Australia katika Uzito wa Super Feather katika pambano lililofanyika New South Wales, Australia tarehe 13 Oktoba, 2018;

v. Iddi Pialari alimdunda Wilson Masumba wa Malawi na kutwaa mkanda wa UBO Africa Welterweight kwa TKO katika mzunguko wa tano, Jijini Dar es Salaam tarehe 26 Januari, 2019;

vi. Bruno Melchiory a.k.a Vifuaviwili alimchanachana Joel Brunker wa Australia na kutwaa mkanda wa IBF Pan Pacific Super Featherweight, Windor, Australia tarehe 9 Machi, 2019;

vii. Hassan Mwakinyo alimkung'uta Sergio Gonzalez wa Nicaragua kwa KO katika mzunguko wa tano katika mchezo uliofanyika Jijini Nairobi, Kenya tarehe 13 Machi, 2019; na

viii. Iddi Mkwela alimchakaza Nicholaus Mwangi wa uzito wa Super Lightweight nyumbani kwao Kenya kwa TKO katika mzunguko wa pili, Jijini Nairobi tarehe 23 Machi, 2019.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati wanamichezo wote nchini kwa kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika mashindano mbalimbali ya kimataifa na hivyo kuitangaza na kuiletea heshima kubwa nchi yetu. Nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na hatua anazochukua kuimarisha michezo nchini. Nimshukuru pia Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu kwa kuipa Wizara yangu ushirikano mkubwa na msaada katika kuendeleza michezo nchini. Pia, niwapongeze watanzania kwa hamasa na uzalendo wanaoonesha kwa timu zetu.

3.2.4.1 Baraza la Michezo la Taifa (BMT)

94. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Michezo la Taifa lilianzishwa kwa Sheria Na. 12 ya mwaka 1967 iliyofanyiwa marekebisho kwa Sheria Na. 6 ya mwaka 1971 pamoja na Sheria Na. 3 ya mwaka 2018. Majukumu ya BMT ni pamoja na kuendeleza na kusimamia ustawi wa aina zote za michezo nchini kwa kushirikiana na Vyama/Mashirikisho ya Michezo na Vilabu.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** Vyama 14, Vilabu 165, Vituo vya Michezo 11 na Mawakala/wakuzaji wa michezo 23 vimesajiliwa. **Kiambatisho Na. XI** ni mwenendo wa usajili wa Vyama, Vilabu, Vituo vya Michezo na Wakuzaji/Mawakala wa Michezo mwaka 2013 – 2018. Aidha, katika

kuhakikisha kunakuwepo utawala bora katika uendeshaji wa shughuli za michezo, marekebisho ya Katiba za Vyama 4, vilabu 7 na Katiba ya Shirikisho la Ngumi za Wazi (OBFT) yamefanyika. Pia, chaguzi 9 za Mashirikisho/ Vyama vya michezo ambazo ni Chama cha Mchezo wa Gofu Tanzania (TGU), Chama cha Kuogelea Tanzania (CHAKUTA), Shirikisho la Ngumi za Wazi Tanzania (OBFT), Chama cha Baiskeli Tanzania (CHABATA), Chama cha Mieleka Tanzania, Chama cha Mchezo wa *Baseball* na *Softball* Tanzania (TaBSA), Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania, Chama cha Mchezo wa Vishale Tanzania (TADA) na Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA) ziliratibiwa na kusimamiwa.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** migogoro ya Vyama vya *baseball* na *softball,* kriketi, kuogelea, ngumi za kulipwa na mpira wa miguu iliyohusu utawala bora na matumizi mabaya ya fedha ilishughulikiwa. Aidha, mkutano wa viongozi 50 wa Mashirikisho/Vyama vya michezo kwa lengo la kuboresha utendaji kazi, kutoa elimu ya rushwa michezoni pamoja na kutoa elimu ya umuhimu wa wanamichezo kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii uliofanyika tarehe 10 Oktoba, 2018 Jijini Dar es Salaam uliratibiwa.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la

Japan (JICA), yalifanyika mashindano ya wanawake *(ladies first)* ya mchezo wa riadha tarehe 24 - 25 Novemba, 2018. Mashindano hayo ambayo yalishirikisha wanamichezo 169 kutoka Mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar, yalilenga kuibua na kuendeleza vipaji vya riadha kwa wanawake pamoja na kuhamasisha ushiriki wao katika michezo. Aidha, yalifanyika mafunzo ya uongozi na utawala katika michezo kwa wanawake 15 ili kuwajengea uwezo wa kushiriki katika uongozi wa michezo na kuhamasisha ushiriki wa wanawake na watu wenye ulemavu katika michezo.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini ya hali ya michezo nchini katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Lindi, Morogoro, Pwani na Tanga ilifanyika. Tathmini hiyo ilihusu Kamati za Maendeleo za Mikoa na Wilaya, Vyama na Mashirikisho ya Michezo, Wadhamini wa Michezo, Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Michezo na Taasisi za Elimu. Lengo la tathmini hiyo ni kufahamu hali ya michezo katika maeneo husika na kupanga mipango ya maendeleo kwa kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazobainika. Aidha, ukaguzi katika Shule Teule 11 za michezo ili kuona hali halisi ya miundombinu na kushauri namna ya kuiboresha kwa maendeleo ya michezo katika shule hizo ulifanyika.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** mashindano ya Mashirikisho/Vyama vya michezo mbalimbali yaliratibiwa ikiwemo Chama cha Mchezo wa Mbio za Magari, mashindano ya Polisi, mashindano ya Shule za Majeshi, michezo ya Ligi Kuu ya Mpira wa Miguu, Wavu, Vishale, Ngumi za Kulipwa, *Baseball* na *Softball* pamoja na Riadha. Aidha, vibali 81 kwa wanamichezo na Timu za Tanzania kwa ajili ya kuziwezesha kushiriki katika Mashindano ya Kimataifa hususan kwa Kamisheni ya Ngumi za kulipwa, Kriketi, Kuogelea, Riadha, Judo, Mpira wa Miguu, Vishale, Netiboli, Kabbadi, Mpira wa Kikapu, WUSHU, Vituo vya Michezo, *Baseball* na *Softball* vilitolewa.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** ushauri wa kiufundi ulitolewa kwa Timu za Tanzania za Michezo ya Karate, Riadha, Mpira wa Miguu na Netiboli ambazo zilishiriki kwenye michezo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika Agosti, 2018 nchini Burundi. Aidha, Timu tatu (3) za Netiboli, Riadha na Mpira wa Miguu kwa Wanawake *(Kilimanjaro Queens)* kati ya nne (4) zilizoshiriki zilipata ushindi wa vikombe na medali katika mashindano hayo.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuimarisha mapato ya kugharamia maendeleo ya michezo nchini, Sheria ya Baraza la Michezo Na.12 ya Mwaka 1967 ilifanyiwa marekebisho na Sheria Na. 3 ya Mwaka 2018. Katika marekebisho hayo

michezo ya Kubashiri Matokeo ya Michezo *(Sport Betting)* imetambulika kama chanzo cha mapato. Wizara kwa kushirikiana na BMT inaendelea na mazungumzo na waendeshaji na wasimamizi wa michezo hiyo ili mapato ya chanzo hiki yaanze kukusanywa.

3.2.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA

102. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kuimarisha utendaji wa Wizara ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya *e-office* kwa watumishi 113, kuwezesha watumishi saba (7) kupata mafunzo ya Stashahada ya IPSAS yanayotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na kutoa mafunzo kuhusu Tathmini ya Utendaji Kazi kwa Njia ya Uwazi (OPRAS) kwa watumishi 221. Aidha, watumishi 10 wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi. Vilevile, watumishi sita (6) walibadilishwa kada baada ya kujipatia sifa; watumishi watatu (3) walithibitishwa kazini na watumishi 20 waliajiriwa. Hatua nyingine zilizochukuliwa na Wizara ni kujenga ofisi mpya za Wizara katika eneo la Mtumba, Jijini Dodoma na kuwapatia watumishi vitendea kazi muhimu ikiwemo samani za ofisi na kompyuta. Aidha, mifumo ya TEHAMA iliboreshwa na kusimamiwa.

Vilevile, watumishi 84 wa Wizara walihamasishwa na kupima kwa hiari VVU/ UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza kwa lengo la kuimarisha afya zao.

4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

103. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2018/19, pia zimejitokeza changamoto mbalimbali. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi ni pamoja na zifuatazo:-

a) Kuendelea kutozingatiwa kwa nidhamu kwa baadhi ya wasanii katika uendeshaji wa kazi zao. Wizara imeendelea kutoa elimu kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio, televisheni na mitandao ya kijamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili katika kazi za sanaa na filamu. Aidha, pale inapobidi, Sheria zimetumika ili kuhakikisha jamii haiendelei kupotoshwa kutokana na kutozingatiwa kwa maadili kupitia kazi hizo.

b) Kuwepo kwa taarifa za upotoshaji na zinazokiuka Sheria ya Huduma za Habari, Na. 12 ya mwaka 2016 pamoja na maudhui hasi mitandaoni na katika baadhi ya redio na televisheni. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kukutana

na Wahariri wa magazeti mbalimbali kwa lengo la kujadili umuhimu wa kuzingatia Sheria na Kanuni za uandishi wa habari na kutoa elimu ya Kanuni za Mawasiliano ya Posta na Kielektroniki (Maudhui ya Redio na Televisheni) ya 2018 na Kanuni za Mawasiliano ya Posta na Kielektroniki (Maudhui Mtandaoni), 2018.

c) Kuongezeka kwa ushindani katika biashara za huduma za utangazaji na uchapishaji zinazotolewa na TBC na TSN hususan matumizi ya mitandao ya kijamii katika utoaji wa matangazo. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuboresha huduma, kujiimarisha kwa kutumia kikamilifu fursa zitokanazo na habari mtandao pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji.

d) Matumizi mabaya ya miundombinu ya michezo hususan Uwanja wa Taifa wakati wa matukio makubwa na hivyo kusababisha hasara. Kupitia Bunge lako Tukufu nitoe wito kwa watanzania kuendelea kutunza miundombinu ya michezo kwani hugharimu Serikali fedha nyingi kuitunza na kuikarabati. Niwatahadharishe kuwa Serikali haitasita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo.

5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

104. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia maendeleo ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Taasisi zake ambapo majukumu mbalimbali yamepangwa kutekelezwa kama ifuatavyo:

5.1 SEKTA YA HABARI

105. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO itaendelea kuhabarisha Umma kuhusu utekelezaji wa Sera na shughuli za maendeleo za Serikali na kuendelea kutoa na kuhuisha leseni kwa magazeti na majarida. Aidha, Wizara itaratibu na kuimarisha utendaji wa Maafisa Habari Serikalini ili kutoa huduma ipasayo kwa wananchi. Vilevile, kutengeneza mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za vitambulisho na leseni zilizotolewa. Pia ushiriki wa vyombo vya habari kwenye matukio ya Kitaifa utaendelea kuratibiwa

5.1.1 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

106. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni:- kwa kushirikiana na wadau; kuendelea kuimarisha Chaneli ya Utalii *(Tanzania Safari Channel)* kwa kununua vifaa na mitambo, kuimarisha maudhui

na kuhakikisha utoshelevu na weledi wa rasilimaliwatu; kuendelea na upanuzi wa usikivu katika maeneo ya nchi ambayo hayana au usikivu wa redio ni hafifu; kuboresha Studio za Redio na Televisheni kwa kufunga vifaa vya kisasa na kununua mitambo na vifaa vya utangazaji kwa ajili ya matangazo mubashara. Majukumu mengine yatakayotekelezwa ni kununua magari kwa ajili ya shughuli za utangazaji pamoja na kuendelea na ujenzi wa jengo la utangazaji Makao Makuu ya Serikali Jijini Dodoma.

5.1.2 Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)

107. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni itatekeleza majukumu yafuatayo:- kuanza uchapaji wa kibiashara baada ya kukamilika kufungwa kwa mtambo mpya; kuimarisha ubora wa bidhaa na huduma zinazotolewa; kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato na kuimarisha utendaji kazi wa rasilimaliwatu kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu.

5.1.3 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

108. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka itatekeleza majukumu yafuatayo:- kuhamasisha utengenezaji na uzalishaji wa maudhui ya ndani yanayozingatia maadili, mila na desturi za Mtanzania; kuendelea kutoa elimu juu ya

Kanuni za Maudhui Mitandaoni na Kanuni za Maudhui Redioni na kwenye televisheni na kuchukua hatua pale ukiukwaji wa kanuni unapotokea; kuvijengea uwezo vituo vya utangazaji kuhusu namna bora ya kuripoti matukio ya uchaguzi; kutembelea Vituo vya Utangazaji ili kutathmini utekelezaji wa masharti ya leseni na kufuatilia utendaji, weledi na kiwango cha elimu kwa wafanyakazi hususan Waandishi wa Habari na watangazaji. Majukumu mengine ni kuendelea kudhibiti matumizi mabaya ya mitandao, kutoa elimu kwa watazamaji wa televisheni na wasikilizaji wa redio kuhusu wajibu na jinsi ya kulalamika pindi wasiporidhishwa na huduma za utangazaji na kuandaa Mwongozo kwa Vyombo vya Utangazaji juu ya Uandaaji wa Maudhui bora yanayozingatia Sheria na Kanuni za Utangazaji.

5.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

109. ***Mheshimiwa Spika***, majukumu yafuatayo yatatekelezwa:- kuchapisha na kusambaza kitabu cha Maadili kitakachotumika kutoa miongozo ya maadili ya Taifa; kufanya utafiti wa lugha za jamii ambazo ziko katika hatari ya kutoweka au kutozungumzwa za jamii ya Segeju, Vidunda, Zaramo na Burunge; kufanya utafiti na kuhifadhi urithi wa utamaduni usioshikika kwa Mikoa ya

Geita, Mwanza na Shinyanga na kuratibu na kusimamia Maadhimisho ya Uanuai wa Siku ya Utamaduni duniani ambayo huadhimishwa tarehe 21 Mei kila mwaka. Majukumu mengine ni kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Utamaduni katika Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro; kuratibu Kikao Kazi cha Maafisa Utamaduni nchini; kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Kiutamaduni Kikanda na Kimataifa na kuratibu, kusimamia na kushiriki katika Mikutano, Matamasha, maadhimisho na Makongamano na matukio ya Kitamaduni Kitaifa na Kimataifa. Vilevile, Wizara itakamilisha uhuishaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na kuandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Mkataba wa UNESCO kuhusu Kulinda na Kuhamasisha Uanuai wa Kujielezea Kiutamaduni wa Mwaka 2005 *(Convention on Protection and Promotion of the Diversity of Cultural Expression, 2005).* Aidha, Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika itaendelea kuratibiwa. Hatua nyingine itakayochukuliwa ni kuupatia ufumbuzi mgogoro wa eneo la asili la shughuli za kijadi la jamii ya wamasai lililopo katika Chuo cha Ufundi, Arusha.

5.2.1 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)

110. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yafuatayo yatatekelezwa:- kuandaa vipindi 600 vya redio na televisheni vya kuelimisha umma kuhusu

matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili; kusanifisha istilahi 300 za nyanja mbalimbali; kutambua na kusajili taasisi na vituo 20 vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni na kuongeza matini za maneno 500,000 za kongoo la Kiswahili. Majukumu mengine ni kuendelea kusajili wataalamu wa Kiswahili katika kanzidata iliyoanzishwa; kuendesha semina 10 kwa waandishi na watangazaji wa redio na televisheni; kutoa mafunzo kwa wataalamu 600 ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni; kuchapisha kamusi kibindo tatu (3) na kufuatilia kwa karibu ukamilishaji wa mwongozo wa kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa kushirikiana na wadau.

5.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA

111. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yafuatayo yatatekelezwa:- kuratibu, kusimamia na kushiriki katika mikutano, matamasha, makongamano na matukio ya sanaa Kitaifa na Kimataifa; kuratibu ushiriki wa wasanii katika Maadhimisho ya Sherehe za Kitaifa (Uhuru na Muungano) na kuratibu Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST). Majukumu mengine ni kufanya tafiti ya Ala za Muziki wa Asili zilizo hatarini kupotea; kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wasanii na wadau wa sanaa kupitia makongamano na mikutano na kuratibu na kuandaa midahalo kuhusu Kampeni ya

Uzalendo na Utaifa kwa wanafunzi wa Vyuo, Shule za Sekondari na Msingi.

5.3.1 Bodi ya Filamu Tanzania

112. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa ni:- kuendelea na zoezi la kutunga Sera ya Filamu; kupitia na kuchambua Miswada 180 ya kutengeneza picha jongevu, makala za filamu, matangazo ya biashara na michezo ya kuigiza; kuhakiki, kupanga katika madaraja na kutoa vibali kwa kazi za picha jongevu (DVD) 1,000 na kubaini, kuimarisha, kuendeleza na kutoa ithibati za uendeshaji wa shughuli za picha jongevu kwa Makampuni, maeneo/miundombinu ya masoko 100, maeneo yasiyo rasmi 5,000 na watendaji wa Sekta ya Filamu na Michezo ya Kuigiza. Aidha, itaendesha operesheni 36 dhidi ya kazi za filamu zinazoingia sokoni kinyume cha taratibu; kuratibu na kuendesha Tamasha la Filamu na Tuzo la Kimataifa *(Serengeti International Film Festival and Award),* kuwajengea uwezo wadau kupitia mafunzo, matukio/makongamano ndani na nje ya nchi na kuanza maandalizi ya ujenzi wa Eneo Changamani la Filamu *(Multipurpose Film Complex)* Jijini Dodoma. Vilevile, kubuni na kuimarisha vyanzo mbalimbali vya mapato ya Bodi.

Pia itaka milisha utungaji wa Kanuni za Sheria ya

Filamu na Michezo ya Kuigiza (Vituo, Maktaba na Maeneo ya Kuonyesha na Kusambazia Picha Jongevu isipokuwa Majumba ya Sinema) za mwaka 2019, urasimishaji wa maeneo yasiyokuwa rasmi kwa lengo la kutanua wigo wa soko; kuitangaza Tanzania kama eneo mahsusi na lenye mandhari ya kipekee katika upigaji picha za filamu, makala za filamu na matangazo; na kuratibu na kusimamia Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) kwa ushirikiano wa Wizara na wadau.

5.3.2 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)

113. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yafuatayo yatatekelezwa:- kuboresha ubunifu pamoja na kuibua na kukuza vipaji vya sanaa nchini; kuwawezesha wasanii kutumia fursa za kiteknolojia katika kuendesha shughuli za sanaa na utafutaji wa masoko na kuongeza uhifadhi wa nyaraka na kumbumkumbu za kazi za sanaa na wasanii. Majukumu mengine ni kutambulisha na kuitangaza Sekta ya Sanaa ndani na nje ya nchi; kuboresha mahusiano ya kiutendaji kati ya Baraza na mamlaka nyingine zinazoratibu masuala ya sanaa ndani na nje ya nchi na kuboresha, kuimarisha na kuongeza vyanzo vya mapato. Vilevile, Baraza litaimarisha mifumo ya utoaji taarifa na huduma; kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa maonyesho na kusimamia maadili katika

sekta ya Sanaa. BASATA kwa kushirikiana kwa karibu na Kampuni ya Clouds Media International, itahamasisha vijana kwa wazee wenye vipaji mbalimbali kushiriki katika mashindano ya kuibua vipaji ya ukanda wa Afrika Mashariki *(East Africa's GOT TALENT)* yatakayofanyika nchini kuanzia mwezi Mei, 2019.

5.3.3 Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)

114. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yafuatayo yamepangwa kutekelezwa:- kuongeza udahili wa wanachuo kutoka idadi ya wanachuo 300 mwaka 2018/19 hadi wanachuo 380 kwa mwaka 2019/20 na kuimarisha ubora katika kujifunza na kufundisha. Aidha, itaimarisha ushirikiano na wadau wa sanaa ndani na nje ya nchi kwa kuendesha warsha na kubadilishana utaalamu, wanachuo na wakufunzi; kuandaa miradi ya kuimarisha taaluma na miundombinu ya Taasisi na kuanzisha mitaala mipya ya sanaa na utamaduni. Majukumu mengine ni kuratibu Tamasha la 38 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni na kutoa ufadhili wa ada ya masomo kwa wasanii wa kike 10. Ufadhili huo utatolewa pia kwa wasanii wawili (me na ke) kutoka kila nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuvutia wasanii kuja kupata maarifa ya sanaa na utamaduni kwa kuwa Taasisi hii ni Kituo cha Jumuiya ya

Afrika Mashariki Chenye Ubora Uliotukuka *(EAC Centre of Excellence)* katika kufundisha sanaa na utamaduni.

5.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

115. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa ni:- kuratibu ukamilishaji wa uhuishwaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995; kusimamia uendeshaji wa Viwanja vya Taifa na Uhuru na kuendelea kutoa huduma za Kinga na Tiba kwa wanamichezo. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, kuboresha miundombinu na vifaa vya michezo katika shule teule za michezo nchini pamoja na kuendelea kutoa mafunzo ya taaluma za michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Ili kufikia malengo yake Wizara itaendeleza mahusiano mazuri iliyoanzisha na wadau ikiwemo sekta binafsi katika kutunza na kuendeleza michezo na miundombinu yake. Mfano ni uhusiano kati ya Wizara na Kampuni ya Azam ambayo katika maandalizi ya michuano ya AFCON kwa vijana chini ya umri wa miaka 17, Kampuni hiyo iliruhusu kiwanja chake kutumika na kukifanyia ukarabati mkubwa ili kukidhi viwango vya kimataifa. Mfano mwingine ni Kampuni ya SportPesa iliyoingia makubaliano na Wizara kuweka nyasi mpya Uwanja wa Taifa na kusimamia utunzaji wake kwa kipindi cha miaka miwili; kuandaa SportPesa

Super Cup kila mwaka kuanzia mwaka 2017 na kuwezesha klabu ya Ligi Kuu ya Uingereza, Everton FC kushiriki katika fainali za kikombe hicho na sasa tuko kwenye maandalizi ya kuikaribisha timu ya Sevilla inayoshiriki Ligi Kuu ya Hispania (La Liga) kuja nchini mwishoni mwa mwezi Mei, 2019 kucheza mechi moja ya kirafiki na kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania. Wizara yangu itashirikiana kwa karibu na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kufanikisha ziara hiyo.

Vilevile, Kampuni ya MultiChoice Tanzania kupitia programu yake ya *Project National Anthem* kwa miaka mitatu (3) sasa, inadhamini mchezo wa riadha ambapo kumekuwa na mafanikio mbalimbali ikiwemo kumuwezesha mkimbiaji wetu Alphonce Simbu ambaye amepata mafanikio makubwa katika riadha ikiwa ni pamoja na kushinda Medali ya Dhahabu katika Mumbai Marathon 2017. Kampuni hii pia imedhamini timu ya Taifa ya Mbio za Nyika iliyoshiriki katika mashindano ya Dunia yaliyofanyika mwezi Machi, 2019 nchini Denmark na kutuwezesha kama nchi kupeleka timu kubwa zaidi katika mashindano hayo ya dunia.

Aidha, natoa shukrani maalum kwa wafanyabiashara wawili, Mzee Reginald Mengi (Mwenyekiti wa makampuni ya IPP) na Mzee Subhash Patel (Mwenyekiti wa Shirikisho la

wenye viwanda Tanzania - CTI) kwa msaada mkubwa waliotoa kwa Timu yetu ya Taifa ya Vijana na kwa Wizara. Mzee Mengi ni Mlezi wa Serengeti Boys ambaye anailea timu hii kwa hali na mali. Ushiriki wetu kwenye kombe la COSAFA kwa kiasi kikubwa uliwezeshwa na mlezi, Mzee Mengi. Mzee Subash Patel yeye ametupatia katoni 11,000 za maji na juisi, ametoa kwa maafisa wa CAF vyumba 27 vya kulala na vingine kufanyia kazi (ofisi) katika hoteli ya nyota 5 ya Sea Cliff kwa kipindi chote cha mashindano haya ya AFCON na ameturuhusu tuweke timu za nchi tatu hoteli ya Whitesands kwa siku 14 bila malipo! Nikishindwa kutambua mchango huo adhimu katika hotuba yangu, basi nitakuwa nanyemelewa na roho ya kichawi.

Vilevile, nizishukuru Kampuni za Sahara Energy na Engen kwa msaada wa mafuta ya magari yote yaliyotumika katika mashindano ya AFCON-U17. Aidha, nimshukuru msanii Rayvanny kwa kuitangaza Timu ya Taifa Stars na pia kujitolea kutumbuiza katika ufunguzi wa mashindano ya AFCON-U17.

5.4.1 Baraza la Michezo la Taifa (BMT)

116. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20 majukumu yafuatayo yatatekelezwa:- kusajili Vyama/Mashirikisho ya Michezo 10, Vilabu 80, Vituo vya Michezo 5 na Wakuzaji wa

Michezo 15; kuratibu na kusimamia ushiriki wa Timu za Taifa katika Mashindano ya Kimataifa ikiwemo *All Africa Games, Olympic* na *East African Community Games* (*EACG);* kutoa mafunzo ya utawala bora kwa viongozi wa Vyama vya Michezo na kuratibu chaguzi za Vyama vya Kitaifa kwa mujibu wa Katiba zao. Majukumu mengine yatakayotekelezwa ni kukamilisha Mapitio ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa ya mwaka 1967 na kuendeleza Mpango wa Michezo kwa Jamii kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Baraza litaratibu uendeshaji wa michezo mbalimbali nchini pamoja na kuhamasisha ushiriki wa Wananchi katika michezo.

5.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA

117. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yafuatayo yatatekelezwa:- kuendelea kuimarisha utendaji wake ikiwemo kuajiri watumishi wapya 21, kupandisha vyeo watumishi 125 na kubadilisha kada watumishi wanne (4) baada ya kujipatia sifa za muundo. Aidha, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi ili kuimarisha utendaji wao ambapo mafunzo ya muda mrefu na mfupi yatatolewa kwa watumishi 30 ndani na nje ya nchi. Pia upatikanaji wa vitendea kazi utaimarishwa. Vilevile, ikiwa ni hatua ya kushirikisha watumishi katika utendaji wa Wizara, vitafanyika vikao viwili (2) vya Baraza la Wafanyakazi. Watumishi pia wataendelea kuhamasishwa kuhusu kujikinga na VVU/UKIMWI na magonjwa mengine

yasiyoambukiza. Pia mafunzo ya kujiepusha na rushwa mahala pa kazi yatatolewa kwa watumishi 127 wa Wizara na Mkataba wa Huduma kwa Mteja utafanyiwa mapitio ili kuhakikisha unaendana na mahitaji ya sasa ya wateja.

6.0 MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

6.1 MAPATO

118. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2019/20 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Tisa Hamsini na Tisa, Mia Tisa na Tano Elfu (Sh.959,905,000) kupitia vyanzo vyake vinavyokusanya kupitia Idara ya Habari-MAELEZO na Maendeleo ya Michezo. Aidha, kwa upande wa Taasisi saba (7) zilizo chini ya Wizara kiasi kinachokadiriwa kukusanywa ni jumla ya Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia Tatu Ishirini na Nne, Mia Nane na Nne Elfu (Sh.37,324,804,000). **Kiambatisho Na. XII** ni mchanganuo wa maduhuli yanayotarajiwa kukusanywa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2019/20.

6.2 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO

119. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2019/20 Wizara imetengewa bajeti ya Shilingi **Bilioni Thelathini, Milioni Mia Nane Sabini na Tisa, Mia Nne Themanini na Tatu Elfu**

(Sh.30,879,483,000). Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Nne Themanini na Tatu na Sabini na Tatu Elfu (Sh.15,483,073,000),** Matumizi Mengineyo ni **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Tatu Tisini na Sita, Mia Nne Kumi Elfu (Sh.9,396,410,000)** na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Sita (Sh.6,000,000,000). Kiambatisho Na XIII** kinabainisha mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo, Taasisi zilizo chini ya Wizara na Miradi ya Maendeleo.

7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2019/20

120. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2019/20 naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2019/20 ya jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini, Milioni Mia Nane Sabini na Tisa, Mia Nne Themanini na Tatu Elfu (Sh.30,879,483,000)**. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Nne Themanini na Tatu, na Sabini na Tatu Elfu (Sh.15,483,073,000),** Matumizi Mengineyo ni **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Tatu Tisini na Sita, Mia Nne Kumi Elfu (Sh.9,396,410,000)** na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Sita (Sh.6,000,000,000)**.

8.0 SHUKRANI

121. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2018/19 yalichangiwa pia na ushirikiano ambao Wizara iliupata kutoka kwa Wadau mbalimbali. Wadau hao ni pamoja na Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Korea ya Kusini, Morocco, Norway, Sweden, Ujerumani na Urusi. Wadau wengine ni Umoja wa Mataifa hususan Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA) pamoja na Umoja wa Ulaya (EU). Wengine ni AZAM TV, Benki za CRDB na NBC, Kampuni ya Coca-Cola, Multichoice Tanzania LTD, NABAKI Afrika, Shell Tanzania, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), SportPesa, Startimes, IPP, Shabiby Line Bus Service, Clouds Media Group, UCSAF na wengine wengi. Kwa niaba ya Wizara, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana wadau hawa na kuwaomba kuendelea kushirikiana na Wizara katika kuziendeleza Sekta zake za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru Waandishi wa Habari, Wanamichezo na Wasanii kwa mchango wao katika kufikia mafanikio ya Wizara. Aidha, ninaishukuru sana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia “Press A” kwa kuchapa hotuba hii kwa wakati.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: **www.habari.go.tz, www.wananchi.go.tz** na **www.tanzaniangovernment.blogspot.com**.

124. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. I

VYOMBO VYA HABARI (MAGAZETI, REDIO NA TELEVISHENI) VILIVYOSAJILIWA MWAKA 2010 -2018

Mwaka	Idadi ya Magazeti/ Majarida	Idadi ya Vituo vya Redio	Idadi ya Vituo vya Televisheni
2010	8	14	1
2011	41	12	-
2012	29	12	-
2013	36	4	-
2014	23	8	3
2015	39	22	1
2016	26	23	6
2017	161	6	3
2018	42	8	3

***Chanzo**: Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)*

Kiambatisho Na. II

IDADI YA MAENEO YA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA KIMKOA HADI MACHI, 2019

Na	Mkoa	Idadi ya Maeneo ya Urithi wa Ukombozi
1	Arusha	7
2	Dar Es Salaam	74
3	Dodoma	12

Na	Mkoa	Idadi ya Maeneo ya Urithi wa Ukombozi
4	Iringa	8
5	Kagera	2
6	Kigoma	11
7	Kilimanjaro	12
8	Lindi	9
9	Mara	6
10	Mbeya	11
11	Morogoro	11
12	Mtwara	10
13	Mwanza	5
14	Pwani	18
15	Ruvuma	15
16	Singida	15
17	Tabora	19
18	Tanga	8
19	Zanzibar	2
JUMLA		**255**

***Chanzo**: Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo*

NYARAKA NA VIFAA VYA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA VILIVYOTUMIKA WAKATI WA HARAKATI ZA UKOMBOZI

Na.	Nyaraka	Idadi
1.	Vitabu	515
2.	Magazeti	197
3.	Pikipiki	1
4.	King'ora	1
5.	Hotuba za Ukombozi	48
6.	Mashairi ya Ukombozi	5
7.	Picha mnato zinazohusiana na Harakati za Ukombozi	5000
8.	Nyaraka mbalimbali zilizobadilishwa kutoka nchi za *"Nordic"*	940
9.	Nyimbo za Ukombozi	45
10.	Mitambo ya kurusha matangazo iliyotumika wakati wa harakati za ukombozi	5
11.	Majarida	25
	JUMLA	**6,782**

***Chanzo**: Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo*

MISWADA ILIYOPEWA ITHIBATI NA BAKITA MWAKA 2018/19

NA.	JINA LA MSWADA	MTUNZI	MCHAPISHAJI
1.	Tujifunze Kuandika Kitabu cha 2	Bantu Digital	Bantu Digital
2.	Kiswahili Darasa la 4	Bantu Digital	Bantu Digital
3.	Historia ya Kiswahili	DPB Massamba	Kiswahili Dev Ltd
4.	Anapenda Kucheza	Room to Read	Room to Read
5.	Jogoo Mbabe	Room to Read	Room to Read
6.	Paka Goi	Room to Read	Room to Read
7.	Nguo ya Sherehe	Room to Read	Room to Read
8.	Muhogo Mtende	Room to Read	Room to Read
9.	Kudu na Tembo	Room to Read	Room to Read
10.	Inatosha	Room to Read	Room to Read
11.	Usiku Mchana	Room to Read	Room to Read
12.	Akaacha Kukoroma	Room to Read	Room to Read
13.	Hapu na Puto	Room to Read	Room to Read
14.	Kinyago cha Kulinda Bustani	Room to Read	Room to Read

NA.	JINA LA MSWADA	MTUNZI	MCHAPISHAJI
15.	Mti Mdogo	Room to Read	Room to Read
16.	Jogoo Mwikaji	Room to Read	Room to Read
17.	Kijiji Kandokando ya Bahari	Room to Read	Room to Read
18.	Tunu ya Mogau	Room to Read	Room to Read
19.	Soma Usikatae Elimu	Valeriano U. Mtundu	
20.	Badilika Hutabaki kama Ulivyo Sasa	Valeriano U. Mtundu	
21.	Maswali ya Bundi Quiz Kidato cha 3&4	Domician Charles	Bundi Quiz
22.	Maswali ya Bundi Quiz Kidato cha 5&6	Domician Charles	Bundi Quiz
23.	Mashindano ya Jua na Upepo	New Orientations LTD	New Oriantations LTD
24.	Mara Yangu ya Kwanza	Christopher Liundi	

NA.	JINA LA MSWADA	MTUNZI	MCHAPISHAJI
25.	Amani Tanga na Tanzania Yetu	Laura Kiara	
26.	Oxford Concise English-Swahili Dictionary Version 2	Oxford University Press	Oxford University Press
27.	Kiswahili III Kitabu cha Mwanafunzi	Oxford University Press	Oxford University Press
28.	Kiswahili III Kiongozi cha Mwalimu	Oxford University Press	Oxford University Press
29.	Kiswahili IV Kitabu cha Mwanafunzi	Oxford University Press	Oxford University Press
30.	Kiswahili IV Kiongozi cha Mwalimu	Oxford University Press	Oxford University Press
31.	Maisha Halisi	Mpango Mkakati Technologies	Mpango Mkakati Technologies
32.	Muhtasari wa ASDP II	Wizara ya Kilimo	Wizara ya Kilimo
33.	Nani Alaumiwe?	Nchilu Kiyungi	Swahili Cruise Channel Publishers

NA.	JINA LA MSWADA	MTUNZI	MCHAPISHAJI
34.	Kisa cha Mkobo	NOFO LTD	NOFO LTD
35.	Kiswahili Darasa la 3 Kitabu cha Mwanafunzi	Mwanzo Education Publishers	Mwanzo Education Publishers
36.	Kiswahili Darasa la 4 Kitabu cha Mwanafunzi	Mwanzo Education Publishers	Mwanzo Education Publishers
37.	Kiswahili Darasa la 5 Kitabu cha Mwanafunzi	Mwanzo Education Publishers	Mwanzo Education Publishers
38.	Najifunza Kuandika I	Mwanzo Education Publishers	Mwanzo Education Publishers
39.	Najifunza Kuandika II	Mwanzo Education Publishers	Mwanzo Education Publishers

NA.	JINA LA MSWADA	MTUNZI	MCHAPISHAJI
40.	Najifunza Kusoma I	Mwanzo Education Publishers	Mwanzo Education Publishers
41.	Najifunza Kusoma II	Mwanzo Education Publishers	Mwanzo Education Publishers
42.	Kiswahili Katika Vyombo vya Habari ndani na nje ya Tanzania	Victor Elia	TATAKI
43.	Katiba ya THAYAKI	Chama cha THAYAKI	THAYAKI
44.	Haki Haikinai	Gambiwa A. Massubo	
45.	Diwani	Gambiwa A. Massubo	

Chanzo: *Baraza la Kiswahili la Taifa*

VITABU VILIVYOSKANIWA KWA AJILI YA MATINI ZA KONGOOO LA KISWAHILI

Na.	JINA LA KITABU	MWANDISHI	IDADI YA VITABU
1	Kusadikika, Maisha yangu baada ya miaka 50, Adili na Nduguze, Masomo yenye Adili, Siku ya Watenzi wote, Utu Bora Mkulima,Wasifu wa Siti Binti Saadi na Kufikirika.	Shaaban Robert	8
2	Kuli, Vuta Nikuvute, Mbali na Nyumbani, Kasri ya Mwinyifuadi na Haini.	Adam Shafi	5
3	Asali Chungu, Babu Alipofufuka, Dunia mti mkavu, Kiza katika Nuru na Nyuso za Mwanamke.	Said A. Mohamed	5
4	Dunia Uwanja wa Fujo, Gamba la Nyoka, Kichwa Maji, Nagona, Roza Mistika na Mzigile.	Prof. Euphrase Kezilahabi	6

5	Ujamaa, Tunu na Raia, Binadamu na Maendeleo, Azimio la Arusha Baada ya Miaka Kumi.	Mwalimu Julius K. Nyerere	4
6	Siri ya sifuri na Kosa la Bwana Musa	Prof. Mohamed Abdul	2
7	Pepo ya Mabwege.	Dkt. Harrson G. Mwakyembe	1
8	Almasi za Bandia na Makuadi wa Soko Huria.	Prof. Chachage S. Chachage	2
9	Kawunju Mkuna Ardhi.	G.S. Mapunda	1
10	Adha ya Heri.	T. Shayo	1
11	Mzalendo.	Prof. Senkoro FMK	1
12	Lwitiko.	M. Mvungi	1
13	Nyota ya Rehema.	Mohamed S. Mohamed	1

Chanzo: *Baraza la Kiswahili la Taifa*

Kiambatisho Na. VI

VIBALI VYA UTAYARISHAJI WA FILAMU NA PICHA JONGEVU VILIVYOTOLEWA MWAKA 2013/14 - 2018/19

Mwaka	Kampuni za Kitanzania	Kampuni za Wageni	Jumla
2013/14	33	125	158
2014/15	36	133	169
2015/16	31	137	168
2016/17	30	123	153
2017/18	46	137	183
2018/19	22	99	121

Chanzo: *Bodi ya Filamu Tanzania*

Kiambatisho Na. VII

FILAMU ZA NDANI NA NJE YA NCHI ZILIZOHAKIKIWA NA KUPEWA VIBALI MWAKA 2013/14 - 2018/19

Mwaka	Filamu za Kitanzania	Filamu za Kigeni	Jumla kwa Mwaka
2013/14	1,181	58	1,239
2014/15	1,339	61	1,400
2015/16	653	114	767
2016/17	706	92	798
2017/18	762	148	910
2018/19[1]	821	140	961

Chanzo: *Bodi ya Filamu Tanzania*

TUZO MBALIMBALI ZILIZOTOLEWA KWA WANATASNIA WA KAZI ZA FILAMU MWAKA 2013/14 - 2018/19

Mwaka	Tuzo za Ndani ya Nchi	Tuzo Kutoka Nje ya Nchi	Jumla kwa Mwaka
2013/14	7	1	8
2014/15	12	1	13
2015/16	11	4	15
2016/17	12	0	12
2017/18	30	10	40
2018/19[2]	39	3	42

Chanzo: *Bodi ya Filamu Tanzania*

WANAFUNZI WALIOHITIMU ASTAHASHADA NA STASHAHADA TaSUBa MWAKA 2010-2018

Mwaka	Wanaume	Wanawake	Jumla	% Wanaume	% Wanawake
2010	28	14	42	67	33
2011	27	8	35	77	23
2012	25	10	35	71	29
2013	32	12	44	73	27
2014	23	12	35	66	34
2015	37	23	60	62	38
2016	31	19	50	62	38
2017	38	6	44	86	14
2018	96	22	118	81	19
JUMLA	**337**	**126**	**463**	**73**	**27**

Chanzo: *Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo*

Kiambatisho Na. X

WANAFUNZI WALIOSAJILIWA KATIKA CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA 2010-2018

Mwaka	Wanaume	Wanawake	Jumla
2010	NA	NA	NA
2011	25	14	39
2012	NA	NA	NA
2013	26	14	40
2014	NA	NA	NA
2015	29	24	53
2016	31	15	46
2017	94	31	125
2018	110	31	141
Jumla	**256**	**137**	**443**

Chanzo: *Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya*

Kiambatisho Na. XI

VYAMA, VILABU, VITUO VYA MICHEZO NA WAKUZAJI/MAWAKALA WA MICHEZO VILIVYOSAJILIWA KUANZIA MWAKA 2013 – 2018

Mwaka	Vilabu vya Michezo	Vyama vya Michezo	Vituo vya Michezo	Wakuzaji/ Mawakala wa Michezo
2013	285	37	12	-
2014	464	17	7	-
2015	224	15	12	-
2016	331	9	15	-
2017	288	29	13	14
2018	212	23	18	29

Chanzo*: Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Michezo (BMT)*

MADUHULI YANAYOTARAJIWA KUKUSANYWA NA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA 2019/20

a. Maduhuli Yanayokusanywa na Wizara

Idara ya Maendeleo ya Michezo

Kijifungu	**Maelezo**	**Makadirio ya Mapato Mwaka 2018/19**	**Makadirio ya Mapato Mwaka 2019/20**
140259	Mapato ya Viwanja vya Michezo (Uhuru na Taifa)	650,000,000	450,000,000
140315	Ada za Mafunzo	58,800,000	259,900,000
140368	Mapato kutoka vyanzo mbalimbali	1,000	1,000
140370	Marejesho ya fedha za Umma	1,000	1,000
Jumla Ndogo		**708,802,000**	**709,902,000**

Kijifungu	Maelezo	Makadirio ya Mapato Mwaka 2018/19	Makadirio ya Mapato Mwaka 2019/20
Idara ya Habari			
140387	Vitambulisho vya Waandishi wa Habari	35,000,000	35,000,000
140202	Machapisho ya picha, mabango na majarida	52,500,000	15,000,000
140265	Ukumbi wa Mikutano	31,500,000	1,000
140264	Usajili wa Magazeti	50,000,000	50,000,000
140310	Ada ya mwaka ya Magazeti	200,000,000	150,000,000
140368	Mapato kutoka vyanzo mbalimbali	1,000	1,000
140370	Marejesho ya fedha za Umma	1,000	1,000
	Jumla Ndogo	**369,002,000**	**250,003,000**
	JUMLA KUU	**1,077,804,000**	**959,905,000**

b. Maduhuli Yanayokusanywa na Taasisi zilizo Chini ya Wizara

Na	Jina la Taasisi	Makadirio ya Mapato 2018/19	Makadirio ya Mapato 2019/20
1.	Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)	11,940,540,000	10,163,000,000
2.	Kampuni ya Magazeti ya Tanzania (TSN)	18,725,500,000	24,996,514,000
3.	Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)	240,500,000	235,190,000
4.	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)	427,000,000	456,446,000
5.	Bodi ya Filamu Tanzania	860,000,000	853,574,000
6.	Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)	478,080,000	540,080,000
7.	Baraza la Michezo la Taifa (BMT)	90,000,000	80,000,000
JUMLA		**32,761,620,000**	**37,324,804,000**

MGAWANYO WA BAJETI YA WIZARA YA MWAKA 2019/20 KWA IDARA NA VITENGO, TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA NA MIRADI YA MAENDELEO

a) Mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo

Kifungu	Idara/ Kitengo	Makisio ya Bajeti Mwaka 2019/20		Jumla
		Mishahara (PE)	Matumizi Mengineyo (OC)	
1001	Utawala na Rasilimali Watu	1,178,731,000	3,024,380,000	4,203,111,000
1002	Fedha na Uhasibu	271,583,000	71,177,000	342,760,000
1003	Sera na Mipango	257,514,000	140,143,000	397,657,000

Kifungu	Idara/ Kitengo	Makisio ya Bajeti Mwaka 2019/20		Jumla
		Mishahara (PE)	Matumizi Mengineyo (OC)	
1004	Mawasiliano Serikalini	70,189,000	48,356,000	118,545,000
1005	Ununuzi na Ugavi	132,940,000	60,911,000	193,851,000
1006	Ukaguzi wa Ndani	70,070,000	47,083,000	117,153,000
1007	TEHAMA	153,868,000	133,035,000	286,903,000
1008	Huduma za Sheria	68,285,000	28,656,000	96,941,000
6001	Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa	438,072,000	220,204,000	658,276,000
6004	Maendeleo ya Michezo	633,071,000	385,127,000	1,018,198,000

Kifungu	Idara/ Kitengo	Makisio ya Bajeti Mwaka 2019/20		Jumla
		Mishahara (PE)	Matumizi Mengineyo (OC)	
6005	Maendeleo ya Sanaa	-	227,409,000	227,409,000
7003	Habari	656,042,000	276,032,000	932,074,000
JUMLA		**3,930,365,000**	**4,662,513,000**	**8,592,878,000**

b) Mgawanyo wa Bajeti kwa Taasisi zilizo Chini ya Wizara

Jina la Taasisi	Makisio ya Bajeti Mwaka 2019/20		
	Mishahara (PE)	Matumizi Mengineyo (OC)	Jumla

6001-280514 Bodi ya Filamu Tanzania (BFT)	217,140,000	46,428,000	263,568,000
6001- 280515 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)	644,142,000	23,208,000	667,350,000
6001-280516 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)	742,629,000	23,213,000	765,842,000
6001 - 280328 – Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)	1,120,220,000	23,211,000	1,143,431,000
6004 – 280518 Baraza la Michezo la Taifa (BMT)	410,539,000	348,198,000	758,737,000
6004 – 270380 Chuo cha Maendeleo ya Michezo-Malya	-	69,639,000	69,639,000

7003 – 280577 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)	8,418,038,000	4,200,000,000	12,618,038,000
Jumla	**11,552,708,000**	**4,733,897,000**	**16,286,605,000**

c) Miradi ya Maendeleo

Na.	**Jina la Mradi**	**Makisio ya Bajeti 2019/20**
Idara ya Habari		
1	4279 - Upanuzi wa Usikivu TBC	5,000,000,000
2	6567 – Habari kwa Umma	1,000,000,000
JUMLA		**6,000,000,000**